Maelezo ya

# Nyakati saba za kanisa

## Sura ya Nane

## The Philadelphian Church Age

Ufunuo 3:7-13

*Na kwa malaika wa kanisa lililoko Filadelfia andika; Haya ndiyo anenayo Yeye aliye mtakatifu, aliye wa kweli, aliye na ufunguo wa Daudi, Yeye Mwenye kufungua wala hapana afungaye, naye afunga wala hapana afunguaye.*

*Nayajua matendo yako. Tazama, nimekupa mlango uliofunguliwa mbele yako, ambao hapana awezaye kuufunga, kwa kuwa unazo nguvu kidogo, nawe umelitunza Neno Langu, wala hukulikana Jina Langu.*

*Tazama, nitawafanya wao walio wa Sinagogi la Shetani, wasemao kwamba ni Wayahudi, nao sio, bali wasema uongo. Tazama, nitawafanya waje kusujudu mbele ya miguu yako, na kujua ya kuwa nimekupenda.*

*Kwa kuwa umelishika Neno la subira Yangu, Mimi Nami nitakulinda, utoke katika saa ya kujaribiwa iliyo tayari kuujilia ulimwengu wote, kuwajaribu wakaao juu ya nchi.*

*Tazama, naja upesi. Shika sana ulicho nacho, asije mtu akaitwaa taji yako.*

*Yeye ashindaye, nitamfanya kuwa nguzo katika hekalu la Mungu Wangu, wala hatatoka humo tena kabisa, Nami nitaandika juu yake Jina la Mungu Wangu, na jina la mji wa Mungu Wangu, huo Yerusalemu Mpya, ushukao kutoka mbinguni kwa Mungu Wangu, Nami nitaandika juu yake Jina Langu jipya.*

*Yeye aliye na sikio, na alisikie Neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa.*

### FILADELFIA

Filadelfia ilikuwa maili sabini na tano kusini mashariki mwa Sardi. Ulikuwa ndio mji wa pili kwa ukubwa katika Lidia. Ulikuwa umejengwa juu ya vilima vingi katika wilaya iliyokuwa maarufu sana kwa kilimo cha divai. Sarafu zake zilikuwa na kichwa cha Bakasi na sanamu ya Bakante (kuhani mwanamke wa Bakusi). Wenyeji wa mji huo walikuwa ni pamoja na Wayahudi, Wakristo wa asili ya Kiyahudi, na waongofu kutoka kwenye upagani. Mji huo ulipatwa na matetemeko ya ardhi ya mara kwa mara, walakini muda wake wa kudumu ulikuwa ni mrefu zaidi kati ya ile miji saba ya Ufunuo. Kusema kweli mji huo ungali uko chini ya jina la Kituruki la Alasehir, ama Mji wa Mungu.

Chapa za hizo sarafu zinadokeza mungu wa mji huo kuwa ni Bakasi. Sasa Bakasi ni sawa na Ninasi ama Nimrodi. Yeye ni „yule anayeombolezewa", ingawa wengi wetu tunamfikiria kuhusiana na ulafi na ulevi.

Ni mwanga wa jinsi gani unaoletwa kwenye mioyo yetu na jambo hili. Hii hapa sarafu ikiwa na mungu katika upande mmoja na kuhani mwanamke ama nabii wa kike upande huo mwingine. Sasa pindua sarafu. Je! kuna tofauti yo yote ya upande itakaoshukia? La, bwana, bado ni sarafu ile ile. Hiyo ni dini ya Kirumi ya Yesu na Mariamu.

Lakini hatufikirii juu ya Rumi tu. La, haiko tu na yule kahaba mkuu. Hasha; kwa maana yeye, kwa uasherati wake mwingi amepata watoto. Mabinti zake sasa ni sarafu za chapa ile ile. Hapo kwenye upande mmoja wa sarafu wamechora ibada ya Yesu na kwenye upande huo mwingine wana kuhani wao wa kike ama nabii wa kike pia naye anaandika kanuni zake za imani na masharti ya dini na mafundisho ya dini na kuyauza kwa watu kwa ajili ya wokovu akikazania ya kwamba yeye na yeye peke yake ndiye aliye na nuru ya kweli.

Ni ajabu jinsi gani kwamba wakati huu una sifa ya sarafu. Kwa maana mama na binti wote wananunua njia yao ya kwenda mbinguni. Pesa wala si damu ndiyo gharama ya kununua. Pesa na wala si Roho ndiyo nguvu inayowasukuma mbele. Mungu wa ulimwengu huu (mali) amepofusha macho yao.

Lakini matendo yao katika mauti yatakwisha hivi karibuni, kwa maana huu ndio wakati ambao Roho analia, "Tazama, naja upesi". Hata hivyo, njoo upesi, Bwana Yesu!

### WAKATI

Wakati wa Kanisa la Filadelfia ulidumu kutoka 1750 hadi yapata 1906. Wakati huu, kwa sababu ya maana ya jina la huo mji, umeitwa Wakati wa Upendano wa Ndugu, kwa kuwa Filadelfia inamaanisha,

"upendano wa ndugu".

## MJUMBE

Mjumbe wa wakati huu bila shaka alikuwa John Wesley. John Wesley alizaliwa huko Epworth, Juni 17, 1703 na alikuwa mmoja wa watoto kumi na tisa waliozaliwa na Samweli na Susanna Wesley. Baba yake alikuwa kasisi katika Kanisa la Kianglikana; lakini kuna uwezekano zaidi kwamba mwelekeo wa kidini wa moyo wa Wesley ulikuwa zaidi sana na msingi wake kwenye mfano wa maisha mema ya mama yake kuliko kwenye theolojia ya baba yake. Yohana alikuwa msomi hodari. Ilikuwa wakati alipokuwa huko Oxford ambapo Yeye pamoja na Charles waliposjiunga na kundi fulani ambalo lilikuwa likifanya ibada za kiroho za kuabudu katika msingi wa kuishi maisha ya ile kweli kwa matendo badala ya kufanya mafundisho yawe ndiyo kielelezo chao. Waliandika mwongozo wa matendo ya kiroho, kama vile kuwapa maskini, kwenda kuwaona wagonjwa na walio kifungoni. Kwa ajili ya jambo hili waliitwa Wamethodisti, na vyeo vingine vya dhihaka. Sasa John alikuwa amejawa sana moyoni na ono lake la haja ya dini kwa ajili ya watu wa ulimwengu kupata dini hivi kwamba akaenda Marekani (Georgia) kama mmishenari miongoni mwa Wahindi. Alipokuwa akisafiri akienda zake kule aliona kwamba wengi wa abiria wa meli aliyosafiria walikuwa ni Wamorevia. Alivutiwa sana na upole wao, amani, na ujasiri katika hali zote. Juhudi zake kule Georgia mbali na yeye kujinyima na kazi ngumu zilikuwa ni kazi bure. Alirudi Uingereza akilia, "Nilienda Marekani kuwaongoa Wahindi lakini jamani! ni nani atakayeniongoa mimi?"

Akirudi London alikutana tena na Wamoravia. Ilikuwa ni Peter Boehler aliyemwonesha njia ya wokovu. Alizaliwa kweli kabisa mara ya pili jambo ambalo lilimfadhaisha sana na kumkasirisha dhahiri ndugu yake, Charles, ambaye hakuweza kuelewa jinsi mtu wa kiroho namna hii kama John angesema hakuwa sawa na Mungu siku za nyuma. Walakini, haukupita muda mrefu, baada ya jambo hilo Charles, pia, aliokolewa kwa neema.

Wesley sasa akaanza kuhubiri Injili hapo London kwenye mimbara zile ambazo hapo awali alikuwa amekubaliwa; lakini haikupita muda wakamwondosha. Katika wakati huu huu ndipo ambapo rafiki yake wa siku nyingi, George Whitefield, alimsaidia sana kwa kuwa alimwalika John aje amsaidie kuhubiri kwenye maeneo ya viwanja ambako maelfu walikuwa wakisikiliza Neno. Kwa mara ya kwanza Wesley aliona ni vigumu ya kwamba eti anapaswa kuhubiri huko nje hadharani badala ya kuhubiri kwenye jengo, lakini wakati alipouona msongamano wa watu na kuona Injili ikifanya kazi katika nguvu za Roho aliyageukia mahubiri ya namna hiyo kwa moyo wake wote.

Mara kazi ilipanuka sana hivi kwamba akaanza kuwatuma waamini wengi wa kawaida waende kuhubiri Neno. Jambo hili lilionekana linaenda sambamba na Pentekoste ambapo Roho aliwainua karibu kwa usiku mmoja watu waliokuwa na nguvu za kuhubiri na kufundisha Neno.

Kulikuwa na upinzani mkali kwa kazi yake lakini Mungu alikuwa pamoja naye. Matendo ya Roho yalidhihirishwa sana na mara nyingi roho ya ushawishi iliwashika watu hata ikawaondolea nguvu zao na wangeanguka chini wakilia kwa huzuni kuu juu ya dhambi zao.

Wesley alikuwa mtu mwenye nguvu sana. Anasema habari zake mwenyewe ya kwamba hawezi kukumbuka kusikia udhaifu wa nafsi hata kwa muda wa robo saa tangu alipozaliwa. Alilala si zaidi ya masaa sita kwa siku; aliamka kwa wakati kuanza kuhubiri karibu miaka mitano kila siku ya huduma yake; alihubiri hadi mara nne kwa siku moja ili kwamba katika mwaka mmoja awe na wastani wa mahubiri zaidi ya 800.

Alisafiri maelfu na maelfu ya maili kama walivyofanya wale wahubiri wake wazungukao huku na huko kupeleka Injili karibu na mbali. Kwa kweli Wesley alisafiri maili 4500 kwa mwaka kwa farasi.

Alikuwa anaamini katika uweza wa Mungu naye aliwaombea wagonjwa akiwa na imani kubwa na akapata matokeo mazuri sana.

Mingi ya mikutano yake iliona madhihirisho ya karama za Kiroho.

Wesley hakupendelea madhehebu. Washirika wake kweli walikuwa na "Shirika la Muungano" ambalo lilikuwa, "kundi la watu waliokuwa na mfano, na waliokuwa wakitafuta nguvu za utauwa, waliounganika kusudi wapate kuomba pamoja, kupokea Neno la maonyo, na kutunzana kwa upendo, kusudi wapate kusaidiana kutimiza wokovu wao wenyewe." Sharti la pekee kwa wale waliokuwa wakijiunga nalo lilikuwa kwamba wao wanapaswa kuwa watu, "waliokuwa na shauku ya kuitoroka hasira ijayo, na kuokolewa na dhambi zao." Muda uliposonga mbele waliorodhesha sheria kali zitumiwe katika kuutawala mwili kwa ukali kwa manufaa ya nafsi zao. Wesley alitambua ya kwamba baada ya kifo chake vuguvugu hilo lingeweza kufanywa dhehebu na Roho wa Mungu awaache wawe mauti. Wakati mmoja yeye alisema ya kwamba hakuhofu ya kwamba jina Methodisti litaondoka duniani bali ya kwamba Roho huenda akaruka akaenda Zake.

Wakati wa uhai wake angeweza kupata utajiri mwingi; lakini hakufanya hivyo. Msemo wake alioupenda sana kuhusu pesa ulikuwa, "Pata zote uwezavyo kupata, weka akiba zote uwezavyo kuweka

akiba, kisha gawa zote uwezavyo kugawa." Ingekuwa ni ajabu vipi kwa Wesley kurudi na kuona madhehebu yanayoitwa kwa jina la Methodisti leo. Wao ni matajiri—ni matajiri sana. Lakini uhai na nguvu za John Wesley zinakosekana.

Inapaswa kukumbukwa pia ya kwamba Wesley kamwe hakutaka kujenga kazi fulani juu ya msingi wa kimadhehebu ama wa kundi. Ingawa alikuwa ni Mwarmenia katika imani yake, hakutaka kujitenga na ndugu kwa misingi ya mafundisho. Alikuwa mwanafunzi mzuri wa Yakobo: aliweka msingi wa uzima wake wa milele juu ya imani na matendo, ama kule kuyaishi yale maisha, badala ya kukubali tu kanuni fulani ya imani ama mafundisho ya maneno fulani.

John Wesley alikufa akiwa na umri wa miaka 88 akiwa amemtumikia Mungu ambapo ni watu wachache sana wangethubutu kufikiri wangeweza.

**SALAMU**

Ufunuo 3:7,

> *"Na kwa malaika wa kanisa lililoko Filadelfia andika; Haya ndiyo anenayo Yeye Aliye mtakatifu, Aliye wa kweli, Aliye na ufunguo wa Daudi, Yeye mwenye kufungua wala hapana afungaye, Naye afungaye wala hapana afunguaye."*

Loo, jinsi maneno hayo yalivyo mazuri. Jinsi hata sauti yake ilivyo na fahari. Inafurahisha jinsi gani kufikiri ya kwamba sifa hizo zote zinaweza kutumika kwa mtu mmoja. Ni nani angethubutu kusema mambo kama hayo juu yake ila Yesu Kristo, Bwana wa Utukufu? Ninaamini ufunguo wa kufasiri hasa maana ya kila moja ya vifungu hivi vya maelezo ya ajabu unapatikana katika kifungu cha 9,

> *"Tazama, nitawafanya wao walio wa sinagogi la Shetani, wasemao kwamba ni Wayahuhdi, nao sio, bali wasema uongo; tazama, nitawafanya waje kusujudu mbele ya miguu yako, na kujua ya kuwa nimekupenda."*

Ninasema aya hii ndio ufunguo kwa sababu inahusu Wayahudi ambao daima wamejiita watoto wa Mungu wakiwatenga wengine wote. Walimsulubisha na kumwua Bwana Yesu Kristo. Tendo lao baya lilileta damu yao wenyewe juu ya vichwa vyao kwa karne nyingi. Yote ni kwa sababu walimkataa Yesu kama Masihi wao, Ambaye kweli alikuwa. Kwao Yeye hakuwa yule Anayekuja, wala Mwana wa Daudi; kwao alikuwa ni Beelzebuli, ama mtu asiye haki anayestahili kuangamizwa tu. Lakini sivyo ilivyo. Yeye kweli alikuwa ni Imanueli, Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Yeye kweli ni, Masihi. Hakika, Yeye alikuwa jinsi hasa anavyojiweka kuwa. Huyo hapo, YESU Yule yule—Yesu Kristo yeye yule jana, na leo na hata milele. Yule Mtakatifu aliye katikati ya vile vinara vya taa ndiye Yesu yeye yule Ambaye alitembea kwenye pwani za Galilaya, Ambaye aliwaponya wagonjwa, Ambaye aliwafufua wafu, na Ambaye ingawa analo thibitisho lisiloweza kukanushwa alisulibishwa na kuuawa. Lakini Yeye alifufuka tena, na ameketi kwenye mkono wa kuume wa Ukuu huko juu.

Wayahudi hawakumwita mtakatifu wakati huo. Hawamwiti mtakatifu sasa. Bali Yeye Ndiye MTAKATIFU.

Zaburi 16:10;

> *"Maana hutakuachia kuzimu nafsi Yangu, wala hutamtoa MTAKATIFU Wako aone uharibifu."*

Walitafuta haki yao kulingana na torati na wakashindwa kabisa, kwa maana kwa torati hakuna mtu awezaye kuhesabiwa haki. Kwa torati hakuna mtu awezaye kufanywa mtakatifu. Utakatifu ni wa Bwana.

I Wakorintho 1:30,

> *"Bali kwa YEYE ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi."*

II Wakorintho 5:21, b,

> *"Ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye."*

Ilikuwa ni Kristo au waangamie, nao wakaangamia kwa sababu wao walimkataa Yeye.

Nao watu wa wakati huo kama vile wa siku hizi walikuwa wanafanya kosa lile lile. Kama vile Wayahudi walivyokimbilia utaratibu wa ibada za sinagogi wapate usalama, vivyo hivyo katika Wakati wa Filadelfia walikuwa wanakimbilia kanisani. Si kujiunga na kanisa ndilo jambo muhimu. Uhai huo haumo kanisani. Uhai uko katika Kristo. "Huu ndio ushuhuda kwamba Mungu ametupa uzima wa milele na uzima huu umo katika Mwanawe. Yeye aliye na Mwana yuna uzima, naye asiye na Mwana hana uzima." Mwanadamu hutakaswa na Roho. Roho wa Utakatifu aliyemfufua Yesu katika wafu ndiye anayekaa ndani yetu na kutufanya watakatifu kwa utakatifu Wake.

Huyo hapo amesimama, YULE MTAKATIFU. Nasi tutasimama pamoja Naye tukivikwa haki Yake, takatifu na utakatifu Wake.

Sasa wakati huu ni wakati wa sita. Mbele za Mungu, wakati unakaribia kwisha. Hivi karibuni atarudi. Hivi karibuni kelele zitapigwa wakati atakapokuja,

> *"Na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa."*

Ufunuo 22:11b

Loo! ninafurahi sana ya kwamba utakatifu wangu si wangu mwenyewe. Ninafurahi ya kwamba nimo ndani ya Kristo, pamoja na kuhesabiwa sifa Zake zote za ajabu na za haki, naam, nimewekewa mimi ndani. Mungu abarikiwe milele!

*"Haya ndiyo anenayo Yeye aliye wa kweli."* Sasa neno hili, 'kweli', ni neno zuri sana. Halimaanishi kweli katika maana tu ya kwamba ni kinyume cha uongo. Linanena juu ya Kutimia Kukamilifu kwa wazo fulani ukilinganisha na Kutimia kwa Sehemu.

Kwa mfano tunakumbuka kwamba Yesu alisema katika Yohana 6:32,

> *"Siye Musa aliyewapa chakula kile cha mbinguni, bali Baba Yangu anawapa ninyi chakula cha kweli kitokacho mbinguni."*

Yohana 15:1,

> *"Mimi ndimi mzabibu wa kweli."*

Waebrania 9:24,

> *"Kwa sababu Kristo hakuingia katika patakatifu palipofanyika kwa mikono, ndio mfano wa patakatifu halisi; bali aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu."*

I Yohana 2:8,

> *"Kwa kuwa giza limepita na ile nuru ya kweli sasa inang"aa."*

Kwa kuwa neno hili, kweli, linaeleza Kutimia Kukamilifu ukilinganisha na wazo la Kutimia kwa Sehemu kama ilivyoonyeshwa katika aya hizi, sasa tunaweza kufahamu kuliko tulivyopata kufahamu hapo nyuma kitu chenyewe ukilinganisha na mfano wake na kitu chenyewe ukilinganisha na kivuli chake. Chukua mfano sasa wa mana kutoka mbinguni. Mungu alishusha chakula cha malaika kutoka mbinguni kwa ajili ya Israeli. Lakini chakula hicho hakikuridhisha. Kilikuwa kizuri tu kwa siku moja. Wale waliokila walikuwa na njaa tena kesho yake. Kama kiliachwa mahali fulani kiliharibika. Lakini Yesu ndiye chakula cha KWELI kitokacho mbinguni, ambapo mana ilikuwa ni mfano tu. Na mtu ye yote akila CHAKULA hicho kilichotoka mbinguni hataona njaa tena. Yeye hahitaji kurudi na kukila tena. Hapo alipokila tu, alipata na uzima wa milele. Hiki hapa KITU KILICHO HALISI. Hakuna haja tena ya kivuli. Hakuna haja ya nusu wokovu. Huu hapa WOTE. Kama tu vile Yesu asivyo sehemu ya Mungu; Yeye NI Mungu.

Hakuna mtu angaliweza kukana ya kwamba Israeli walikuwa na nuru. Walikuwa ndio watu pekee waliokuwa na nuru kama taifa. Ni kama wakati Misri ilipokuwa na giza sana kwamba mtu angaliweza kuligusa. Lakini katika nyumba za Waisraeli kulikuwa na nuru. Lakini sasa nuru ya kweli imekuja. Nuru ya ulimwengu ni Yesu. Musa na manabii walileta nuru kwa njia ya Maandiko yanayomhusu Masihi. Kwa hiyo Israeli walikuwa na nuru. Lakini sasa Utimilifu wa nuru umekuja, na kile kilichokuwa Neno lililokuwa linameka kimejitokeza sasa katika Mng"aro wa Mungu akidhihirishwa miongoni mwa watu Wake. Kama vile ile nguzo ya moto ilivyotoa nuru usiku, na jambo hilo lilikuwa ni zuri sana, sasa nuru na uzima vilidhihirishwa katika utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili.

Israeli walikuwa wakichukua mtamba wa ng"ombe mwekundu na kumtoa dhabihu juu ya madhabahu kwa ondoleo la dhambi. Kwa mwaka mzima dhambi za mtu mwenye hatia zilifunikwa. Lakini kufunikwa huko hakungeweza kuondoa tamaa ya dhambi. Haikuwa sadaka kamilifu. Ilikuwa ni kivuli mpaka ile halisi ilipojitokeza. Kwa hiyo kila mwaka mtu huyo angetoa dhabihu na kila mwaka anarudi kwa sababu alikuwa angali na tamaa ile ile ya kutenda dhambi. Uhai wa yule mnyama ulifanya upatanisho kwa ajili ya dhambi zake, lakini kwa kuwa ni damu ya mnyama iliyomwagwa na uhai wa mnyama uliotolewa uhai huo haukuweza kumrudia mtu huyo. Kama ulikuwa umerudi, ungali haungefaa kitu bado. Lakini wakati Kristo yule kibadala kikamilifu alipotolewa, na damu Yake ikamwagwa, basi uzima uliokuwemo ndani ya Kristo ulimrudia mwenye dhambi aliyetubu na uzima huo kwa kuwa ni uzima mkamilifu wa Kristo, usio na dhambi na ni wa haki, basi mwenye hatia angeweza kwenda huru kwa maana hakuwa na tamaa ya kutenda dhambi. Uzima wa Yesu ulikuwa umerudi juu yake.

Hiyo ndiyo maana ya Warumi 8:2,

*"Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti."*

Lakini Wayahudi huko nyuma katika wakati wa Yesu hawakutaka kukubali dhabihu hiyo. Damu ya mafahali na mbuzi haikukamilisha kitu. Wakati mmoja ilikuwa ndiyo njia iliyochaguliwa na Mungu. Lakini sasa Kristo akiisha kutokea katika mwili, na kwa kumwagwa kwa damu Yake Mwenyewe ameondoa dhambi na kwa toleo hilo la nafsi Yake ametufanya sisi kuwa wakamilifu. Wayahudi wasingechukua jambo hilo. Lakini vipi kuhusu ule Wakati wa Filadelfia, na, naam, zile nyakati zingine, pia? Je, kweli walikubali ukweli huu katika Kristo? La bwana. Hata ingawa Luther alileta kweli ya kuhesabiwa haki, Kanisa la Kirumi, na pacha wake wa mashariki, Kanisa la Kiorthodoksi, yangali yalishikilia matendo.

Sasa matendo ni sawa, lakini hayakuokoi. Hayakufanyi wewe mkamilifu. Ni Kristo ama uangamie. Na hata si Kristo NA matendo. Ni Kristo peke yake. Wakati huu ulianzisha miaka ya Uarmenia usioamini katika Kristo kama ALIYE HALISI. Hauimbi juu ya "Hakuna kingine ila ile Damu," kwa maana unaimba juu ya "Hakuna kingine ila damu NA mwenendo wangu mwenyewe." Sasa ninaamini katika mwenendo mzuri. Kama umeokoka utatenda kwa haki. Tayari tumepitia hayo. Lakini hebu niwaambie sasa, wokovu SI Yesu pamoja NA. Ni Yesu PEKEE. WOKOVU NI WA BWANA. Tangu mwanzo mpaka mwisho yote ni MUNGU. Hebu maisha Yake yawe ndani yangu. Hebu na iwe ni damu Yake inayonitakasa. Hebu na iwe ni Roho Wake anayenijaza. Jalia liwe Neno Lake moyoni mwangu na kinywani mwangu. Hebu na yawe ni mapigo Yake yanayoniponya. Hebu na iwe ni Yesu, na Yesu Peke Yake. Si kwa matendo ya haki niliyotenda. La bwana. Kristo ndiye uzima wangu. Amina.

Ninajisikia ningeendelea tu na kuendelea kuhusu kweli hizi, bali nitawapa wazo moja zaidi. Ni kuhusu ule wimbo wa ajabu ambao A. B. Simpson aliandika.

"Wakati mmoja ilikuwa ni baraka,
Sasa ni Bwana.
Wakati mmoja ilikuwa ni kuhisi,
Sasa ni Neno Lake.
Wakati mmoja Karama Yake niliitaka,
Sasa Mpaji Mwenyewe.
Wakati mmoja nilitafuta kuponywa,
Sasa Yeye Mwenyewe Pekee.
Yote katika yote milele,
Nitamwimbia Yesu.
Kila kitu katika Yesu,
Na Yesu kila kitu.

Hakuna kitu cho chote katika maisha haya, hata kiridhishe namna gani, kiwe kizuri na chema vipi, ila utapata jumla ya ukamilifu wote katika Kristo. Kila kitu hufifia kabisa mbele Zake.

*"Yeye Aliye na ufunguo wa Daudi."* Fungu hili la maneno ya kupendeza linafuata na kutoka kwenye fungu lililotangulia, "Yeye aliye wa kweli."_Kristo, Utimilifu Mkamilifu, ukilinganisha na Utimilifu wa Sehemu. Hili hapa. Musa alikuwa nabii fulani wa Mungu, lakini Yesu (kwa mfano wa Musa) alikuwa YULE Nabii wa Mungu. Daudi (mtu aliyempendeza Mungu) alikuwa mfalme wa Israeli, lakini Yesu ni yule Daudi Mkuu Zaidi, Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana, Mungu Aliye Mungu hasa. Sasa Daudi alizaliwa katika kabila la Yuda ambalo kwake hakukutoka makuhani wo wote, hata hivyo alikula mikate ya wonyesho iliyotengwa kwa ajili ya makuhani. Yeye alikuwa shujaa mkuu akishinda adui, akiwaimarisha watu; kama mfalme yeye aliketi kwenye kiti cha enzi. Yeye alikuwa ni nabii. Alikuwa mfano wa ajabu wa Kristo.

Sasa inasema katika Isaya 22:22,

*"Na ufunguo wa nyumba ya Daudi nitauweka begani Mwake; Yeye atafungua wala hapana atakayefunga; Naye atafunga, wala hapana atakayefungua."*

Roho anatumia maneno haya ya Agano la Kale kumhusu Bwana Yesu Kristo na huduma Yake katika kanisa. Kile ufunguo wa Daudi ulichoomaanisha wakati ule ni kivuli tu, ambalo limetimizwa sasa katika Yesu akisimama katikati ya vinara vya taa. Inahusiana na Bwana wetu BAADA ya kufufuka Kwake na si safari Yake ya duniani. Lakini ufunguo huu unaonyesha nini? Jibu liko kwenye MAHALI ufunguo ulipo. HAUKO katika mkono Wake. Haukuvaliwa shingoni Mwake. Haujawekwa mikononi mwa watu wengine, ama hiyo aya haingekuwa inasema ya kwamba YEYE PEKEE NDIYE ANAYEUTUMIA UFUNGUO HUO_KWA MAANA YEYE PEKE YAKE NDIYE ANAYEFUNGUA NA KUFUNGA, WALA HAKUNA MTU aliye na haki hiyo ila Yesu Mwenyewe. Hiyo si ni kweli? Lakini ufunguo uko wapi? UKO BEGANI MWAKE. Lakini BEGA lina uhusiano gani nao?

Soma Isaya 9:6,

*"Na uweza wa kifalme utakuwa begani Mwake."*

Lakini hii inamaanisha nini? Jibu ni hili. Fungu la maneno, "uweza wa kifalme begani Mwake" linatokana na sherehe ya arusi ya Mashariki. Baada ya bibi- arusi kukabidhiwa kwa bwana arusi yeye huondoa shela yake na kuiweka juu ya mabega ya bwana arusi, ikionyesha ya kwamba si kwamba tu yeye yuko chini ya mamlaka yake—ya kwamba amehamisha haki zake akazipeleka kwake—ya kwamba yeye ndiye kichwa—lakini pia ya kwamba yeye ndiye anayewajibika kumwangalia na kumtunza na ya kwamba YEYE NA YEYE PEKE YAKE—HAKUNA MWINGINE— HAKUNA MWANAMUME MWINGINE—HAKUNA MAMLAKA NYINGINE_ILIYO NA HAKI YO YOTE NA JUKUMU. Na huyo, mpendwa, ndiye UFUNGUO wa Daudi. Mungu akiwa Mwenyezi, Yeye alijua tangu zamani kwa uamuzi wa Kiungu ni nani hasa angalikuwa katika bibi-arusi Wake. Yeye alimchagua. Bibi-arusi hakumchagua Yeye. Yeye ndiye aliyemwita. Bibi-arusi hakuja kwa hiari yake. Alikufa kwa ajili yake. Yeye alimwosha katika damu Yake mwenyewe. Alimnunua. Yeye ni mali Yake na ni Wake peke yake. Yeye bibi-arusi amejitoa Kwake kabisa naye Bwana Arusi anakubali wajibu huo. Yeye ndiye kichwa chake, kwa kuwa Kristo ndiye kichwa cha kanisa Lake. Kama vile Sara alivyomwita Ibrahimu, Bwana, hivyo hivyo bibi-arusi anafurahi ya kwamba Yeye ni Bwana wake. Yeye husema na mwanamke hutii kwa kuwa hiyo ndiyo furaha yake.

Lakini je! Watu wamekubali kweli hii? Je! Wao wameuheshimu Utu Wake Ambaye ndiye pekee aliye na mamlaka makamilifu ya kifalme juu ya kanisa Lake? Ninasema, "LA". Kwa sababu katika kila wakati kanisa limekuwa likitawaliwa na serikali ya makasisi—ukasisi—uhalifa wa kimitume—ukifungia mlango wa rehema na neema kwa ye yote utakaye, na badala ya kukubali upendo na jukumu la kanisa serikali hiyo ya makasisi imeliteka nyara kanisa kwa tamaa ya fedha na kuliangamiza. Makasisi waliishi katika anasa wakati kanisa maskini likijilisha kwa makapi ya manyanyaso. Na hakuna hata wakati mmoja uliotenda tofauti. Kila mmoja ulijifunga kwenye madhehebu na kuuweka utawala juu ya wanadamu na kuliweka kanisa chini ya utawala huo. Watu walipothubutu kuinuka, na walisetwa kikatili au kutupwa nje. Kila dhehebu lina roho yule yule. Kila dhehebu huapa ya kwamba ndiyo yaliyo na ufunguo wa kulitawala kanisa. Kila dhehebu linadai kwamba linafungua mlango. Lakini hilo si kweli. Ni Yesu na Yesu, peke yake. Yeye huwaweka washirika katika ule Mwili. Anawapa huduma zao. Anaweka karama ili wazitumie. Yeye humjali na kumwongoza. Bibi-arusi huyo ni mali Yake peke yake na Bwana Arusi hana mwingine ila Yeye.

Jinsi wakati huu wa kanisa tuishio ndani yake ulivyo mbali sana na jambo halisi. Na siku moja mara watu hawa ambao hata sasa wanaonekana kama kwamba wanawakilisha kanisa watainuka katika pilikapilika za ekumeni wamweke mpinga-Kristo aliye hai apate kuongoza madhehebu yao ambayo yanamwondosha Bwana na tutamwona Yeye (Kristo) nje ya kanisa akisema,

> *"Tazama, nasimama mlangoni, nabisha: mtu akiisikia sauti Yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja Nami."*

Ufunuo 3:20.

Lakini hebu niseme jambo hili. Bwana wetu hajashindwa. Watu wanadai kumfungulia Mungu mlango na kuufunga mlango huo, bali wao ni waongo. Wote aliompa Baba watamjia, na kila amwendeaye Yeye hatatupwa nje kamwe; Yeye hatampoteza hata MMOJA wao. Yohana 6:37-39. Na hapo yule mshirika wa mwisho wa mwili wa Kristo atakapoingia, ndipo Bwana wetu atakapotokea.

Ufunguo wa Daudi. Daudi hakuwa mfalme wa Israeli—Israeli yote? Na je! Yesu siye Mwana wa Daudi kulingana na ukweli kwamba Yeye ataketi juu ya kiti cha enzi cha Daudi katika ule utawala wa miaka elfu na kutawala na kuwa na mamlaka juu ya urithi Wake? Hakika. Kwa hiyo ufunguo wa Daudi unaonyesha ya kwamba Yesu Ndiye atakayeleta ule Utawala wa Miaka Elfu. Yeye aliye na funguo za mauti na kuzimu atawafufua walio Wake wapate kushiriki katika utawala Wake wa haki duniani.

Ni ajabu iliyoje kwamba Bwana wetu ana majibu yote. Hakika ndani Yake ahadi zote za Mungu zinatimizwa. Kweli kwa kuwa NDANI Yake sisi ni warithi wa yale ambayo Yeye ametununulia.

Naam, huyo hapo amesimama, Bwana wa Utukufu. Wakati mmoja kama Baba, Yeye alizungukwa na malaika, malaika wakuu, makerubi, na maserafi, na jeshi lote la mbinguni, likilia, "Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu ni Bwana Mungu wa Majeshi." Utakatifu Wake ulikuwa hivi hata hakuna mtu angeweza kumkaribia. Lakini sasa tunamwona kanisani, akishiriki utakatifu Wake pamoja nasi, mpaka katika Yeye tumekuwa haki halisi ya Mungu. Naam, na Huyo hapo amesimama, "Yesu, Mkamilifu kwa Kila Kitu,"—Ua la Bondeni, Nyota ya Asubuhi Inayong"aa, Aliye Mzuri Kuliko Wote kati ya Elfu Kumi, Alpha na Omega, Shina na Mzao wa Daudi, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu—Yote na katika Yote.

Isaya 9:6,

> *"Kwa maana kwa ajili yetu Mtoto amezaliwa, tumepewa Mtoto Mwanamume; na uweza wa kifalme utakuwa begani Mwake; Naye ataitwa Jina Lake, Mshauri wa Ajabu, Mungu Mwenye nguvu, Baba wa Milele, Mfalme wa Amani."*

Ndani Yake mna utimilifu mkamilifu. Ingawa wakati mmoja hatukumheshimu, sasa tunampenda kwa furaha isiyoneneka na iliyojaa utukufu. Amesimama katikati ya kanisa, nasi tutaimba sifa Zake, kwa

maana Yeye Mshindi Mkuu ndiye kichwa cha kanisa ambalo ni bibi-arusi Wake. Yeye alimnunua huyo bibi-arusi. Yeye anamiliki. Yeye ni Wake na wake pekee na Yeye anamjali. Yeye ni mfalme wetu na sisi ni ufalme Wake, milki Yake ya milele.

Sasa mtakumbuka ya kwamba mwanzoni mwa kifungu cha 7, nilisema kifungu cha 9 kingetusaidia kufahamu jambo hilo. Natumaini mliona nilichomaanisha. Yesu anajiweka Mwenyewe kama Yeye Aliye mtakatifu, wa kweli, (ama aliye halisi pekee) Yule aliye na ufunguo wa Daudi, Yeye aliyefungua na kufunga. Na hilo ni kweli kabisa. Hayo mafungu ya maneno yanamwelezea kikamilifu. Lakini Wayahudi katika siku Zake walimkataa Yeye na yote aliyokuwa. Walimkataa Mwokozi wao na yote aliyokusudia kwao. Na Mkristo wa jina sasa amefanya vile vile. Wamefanya yale Wayahudi waliyofanya hasa. Wayahudi walimsulibisha Yeye halafu wakamgeukia mwamini wa kweli. Mkristo wa kawaida amemsulibisha Yeye upya na kuligeukia kanisa la kweli apate kuliangamiza. Lakini Mungu ni wa kweli, na Yeye aliye juu ya yote bado atarudi, na atakaporudi ataonyesha Mwenye Nguvu peke yake ni nani. Na wakati anapojithibitisha Mwenyewe kwa ulimwengu, na ulimwengu wote unasujudu miguuni Pake, wakati huo ulimwengu wote utasujudu miguuni pa watakatifu, ikithibitisha ya kwamba walikuwa sahihi katika msimamo wao pamoja Naye. Mungu na abarikiwe milele!

## WAKATI WA MLANGO ULIOFUNGULIWA

Ufunuo 3:8,

> *"Nayajua matendo yako; tazama, nimekupa mlango uliofunguliwa mbele yako, ambao hapana awezaye kuufunga, kwa kuwa unazo nguvu kidogo, nawe umelitunza Neno Langu, wala hukulikana Jina Langu."*

Fungu la maneno la kwanza la aya hii, "Nayajua matendo yako," linafafanuliwa katika sehemu iliyosalia ya aya hii, kwa maana matendo yao yalikuwa na uhusiano na 'mlango uliofunguliwa,' 'nguvu kidogo,' 'Neno na Jina.'

Kusudi tufahamu utajiri wa maana inayohusika katika "tazama nimeweka mlango uliofunguliwa mbele yako, na hapana awezaye kuufunga," hatuna budi sasa kukumbuka yale yaliyosemwa kuhusu kila wakati kupitiliza na kuingia katika wakati mwingine. Kuna kuingiliana, kuyeyuka ama kufifia na kuishia ndani yake, badala ya kukatika mara moja na kuwa na mwanzo ulio waziwazi. Wakati huu kwa dhahiri unapita na kuingia katika wakati unaofuata. Na si kwamba tu wakati huu unapita na kuingia katika wakati wa mwisho lakini wakati wa mwisho katika mambo mengi ni kuendelea tu kwa wakati wa sita. Wakati wa saba (wakati mfupi sana) unakusanya ndani yake wenyewe kwa ajili ya kazi moja ya haraka, maovu yote ya kila wakati, na hata hivyo unakusanya kweli yote ya Pentekoste. Mara Wakati wa Filadelfia unapokuwa karibu kwisha muda wake, Wakati wa Laodikia unaingia upesi, ukileta magugu pamoja na ngano kwenye mavuno,

> *"Yakusanyeni kwanza magugu mkayachome; bali ngano ikusanyeni ghalani Mwangu."*

Mathayo 13:30.

Kumbukeni, tafadhalini, ya kwamba Wakati wa Sardi ulianzisha yale matengenezo ambayo hayana budi kuendelea mpaka ile mbegu iliyopandwa kule Pentekoste ipitie kwenye mzunguko kamili wa kupanda, kutia maji, kulishwa, nk., mpaka irudi moja kwa moja kwenye punje ya asili. Wakati jambo hili likiendelea, yale magugu yaliyopandwa hayana budi kupitia katika mzunguko wao na yavunwe pia. Hilo ndilo tunaloona likitukia hasa. Kama unaweza tu kufikiria juu ya majira, unaweza kupata picha nzuri sana ya jambo hili. Ule mmea unaouona ukikua katika nguvu nyingi katika majira ya kiangazi mara tu unaonekana ukianza kupooza. Huwezi kujua hasa ni wakati gani majira ya kiangazi yaligeuka yakawa ya masika—yalififia tu yakaishia ndani yake. Hivyo ndivyo nyakati zilivyo, na hasa hizi mbili za mwisho.

Wakati huu ndio Yesu anaouambia, „Naja UPESI" aya ya 11. Hilo linaufanya wakati wa mwisho kuwa mfupi sana. Laodikia ni wakati wa kazi ya haraka. Unafupishwa.

Sasa tutaeleza kwa dhahiri kirefu juu ya MLANGO ULIOFUNGULIWA ambao hapana anayeweza kuufunga. Kwanza kabisa nataka kuelezea kwa kirefu juu ya mlango uliofunguliwa kama uonyeshao juhudi kubwa mno za kimishenari za wakati ule. Paulo aliita jitihada mpya ya kimishenari kwa ajili ya Bwana mlango uliofunguliwa.

II Wakorintho 2:12,

> *"Basi nilipofika Troa kwa ajili ya Injili ya Kristo, nikafunguliwa mlango katika Bwana."*

Kwa hiyo tunaweza kuona kwa kulinganisha Maandiko ya kwamba mlango huu uliofunguliwa ulionyesha kuenezwa kukuu mno kwa Injili ambako ulimwengu ulipata kuona.

Ninawatakeni mwone jambo fulani hapa. Mungu hufanya kazi katika watatu, sivyo? Katika wakati wa tatu ama Wakati wa Pergamo ilikuwa ndipo ambapo kanisa liliolewa na serikali. Matendo ya Wanikolai

yalikwisha kuwa fundisho la Wanikolai. Wakati huo ulikuwa ndio ule MLANGO ULIOFUNGULIWA kwa ajili ya ule mzabibu wa uongo. Mara ulipoungwa mkono na nguvu za serikali ndipo ukawa hasa shirika la kilimwengu hata ingawa ulichukua jina, Mkristo. Kwa hiyo ukaenea kwa kasi kama moto wa mwituni. Lakini sasa, nyakati tatu baadaye, baada ya jitihada za muda mrefu na vita vigumu vya imani, huu hapa unakuja MLANGO ULIOFUNGULIWA kwa ajili ya ile kweli. Neno la Bwana sasa lina siku yake. Hapana shaka ule wakati wa tano ulikuwa umeandaa jukwaa kwa ajili ya ufufuo huu mkuu sana, kwa maana wakati huo ulitupa sisi uvumbuzi wa nchi ngeni, ukoloni, uchapishaji wa vitabu, nk.

Lingekuwa ni jambo zuri sana iwapo huu„mlango uliofunguliwa" ungelifuata kielelezo cha Mungu cha Pentekoste ambacho kiliandikwa katika Waebrania 2:1-4, "Kwa hiyo imetupasa kuyaangalia zaidi hayo yaliyosikiwa tusije tukayakosa. Kwa maana, ikiwa lile Neno lililonenwa na malaika lilikuwa imara, na kila kosa na uasi ulipata ujira wa haki, sisi je! Tutapataje kupona, tusipojali wokovu mkuu namna hii; ambao kwanza ulinenwa na Bwana, kisha ukathibitika kwetu na wale waliomsikia; Mungu Naye akishuhudia pamoja nao kwa ishara na maajabu na nguvu za namna nyingi, na kwa magawanyo ya Roho Mtakatifu, kama alivyopenda Mwenyewe." Sasa unajua ya kwamba hiki ndicho kielelezo kwa maana Yesu, Mwenyewe, alisema hivyo.

Marko 16:15-20,

> *"Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.*
>
> *Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa.*
>
> *Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa Jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya;*
>
> *Watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.*
>
> *Basi Bwana Yesu, baada ya kusema nao, akachukuliwa juu mbinguni, akaketi mkono wa kuume wa Mungu.*
>
> *Nao wale wakatoka, wakahubiri kotekote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kulithibitisha lile Neno kwa ishara zilizofuatana nalo. Amina.*

Yeye hakuwaambia kamwe waende ulimwenguni mwote wakaanzishe vyuo vya Biblia; wala hakuwaambia wakasambaze vitabu. Sasa mambo hayo ni mazuri, lakini yale Yesu aliyowaambia kufanya ilikuwa ni KUIHUBIRI INJILI—kushikilia NENO—ndipo ishara zitafuata. Utangulizi wa kwanza kabisa tulio nao wa jinsi Ufalme wa Mungu ulipaswa uhubiriwe ulikuwa ni wakati Yeye alipowatuma wale thenashara. Katika Mathayo 10:1-8, Yeye aliwaagiza na kuwafundisha hivi,

> *"Akawaita wanafunzi Wake kumi na wawili, akawapa amri juu ya pepo wachafu, wawatoe, na kupoza magonjwa yote na udhaifu wa kila aina.*
>
> *Na majina ya hao mitume kumi na wawili ni haya; Wa kwanza Simoni, aliyeitwa Petro, na Andrea nduguye; Yakobo wa Zebedayo, na Yohana nduguye;*
>
> *Filipo, na Bartholomayo; Tomaso, na Mathayo mtoza ushuru; Yakobo wa Alfayo, na Lebasi ambaye jina la baba yake ni Thadayo;*
>
> *Simoni Mkananayo, na Yuda Iskariote, naye ndiye mwenye kumsaliti.*
>
> *Hao Thenashara Yesu aliwatuma, akawaagiza, akisema, Katika njia ya Mataifa msiende, wala katika mji wo wote wa Wasamaria msiingie.*
>
> *Afadhali shikeni njia kuwaendea kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli.*
>
> *Na mnapoenda, hubirini, mkisema, Ufalme wa mbinguni umekaribia.*
>
> *Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo; mmepata bure, toeni bure."*

Huduma hii aliyowapa Yeye ilikuwa hasa ni kushiriki huduma Yake Mwenyewe pamoja nao, kwa maana inasema katika Mathayo 9:35-38,

> *"Naye Yesu alikuwa akizunguka katika miji yote na vijiji, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri Habari Njema ya ufalme, na kuponya magonjwa yote na udhaifu wa kila aina miongoni mwa watu.*
>
> *Na alipowaona makutano, aliwahurumia, kwa sababu walikuwa wamechoka na kutawanyika kama kondoo wasio na mchungaji.*

*Ndipo alipowaambia wanafunzi Wake, Mavuno kweli ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache. Basi mwombeni Bwana wa mavuno, apeleke watenda kazi katika mavuno Yake."*

Sasa watu wengi wana wazo kwamba ni mitume tu ndio waliopewa huduma hiyo na Bwana wetu Yesu, na kwa hiyo wakati walipokufa, huduma hiyo ilikuwa imekwisha. Sivyo ilivyo.

Hapa katika Luka 10:1-9, tunaona ya kwamba katika siku za safari Yake ya duniani Yeye alikuwa tayari ameanza kuwapa walio Wake huduma za nguvu,

*"Basi baada ya hayo Bwana aliweka na wengine, sabini, akawatuma wawili wawili wamtangulie kwenda kila mji na kila mahali alipokusudia kwenda Mwenyewe.*

*Akawaambia, Mavuno kweli ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache; basi mwombeni Bwana wa mavuno apeleke watenda kazi katika mavuno Yake.*

*Enendeni, angalieni, nawatuma kama wana-kondoo kati ya mbwa- mwitu.*

*Msichukue mfuko, wala mkoba, wala viatu; wala msimwamkie mtu njiani.*

*Na nyumba yo yote mtakayoingia, semeni kwanza, Amani iwemo nyumbani humu,*

*Na akiwamo mwana wa amani, amani yenu itamkalia; la, hayumo, amani yenu itarudi kwenu.*

*Basi, kaeni katika nyumba iyo hiyo, mkila na kunywa vya kwao; maana, mtenda kazi amestahili kupewa ujira wake. Msihame-hame kutoka nyumba hii kwenda nyumba hii.*

*Na mji wo wote mtakaouingia, wakiwakaribisha, vileni vyakula viwekwavyo mbele yenu;*

*Wapozeni wagonjwa waliomo, waambieni, Ufalme wa Mungu umewakaribia."*

Ni nani angethubutu kukanusha huduma kuu sana ya Filipo? Ni nani angethubutu kukanusha huduma kuu za Ireneo, Martin, Columba, Patrick na idadi kubwa isiyohesabika ya wengine waliokuwa na upako wa Mungu juu yao?

Naam. Njia ya Biblia ndiyo njia halisi ya mlango uliofunguliwa. Nami ninataka kuongeza ushuhuda wangu kwa jambo hilo. Sababu ya mimi kufanya jambo hilo ni kwa kuwa ninaweza tu kunena kwa uhakika kuhusu yale Mungu aliyotenda katika maisha yangu mwenyewe. Kwa hiyo kama mtaniwia radhi kwa muhtasari mfupi hapa wa kibinafsi nitawaambia jinsi ninavyojua kwa hakika ya kwamba Yesu ni yeye yule jana na leo na hata milele na kwamba nguvu za Mungu zinapatikana kwa wale watakaoamini na kupokea.

Wakati wa safari yangu ya kimishenari huko Afrika ya Kusini, Mungu alibariki sana hivi kwamba wakati nilipokuja Durban mahali pekee ambapo pangeanza kuwatosha watu palikuwa ni ule uwanja mkubwa sana wa mashindano ya mbio ambao ndio wa pili katika ukubwa duniani. Umati ulikuwa umezidi 100,000. Ili kudumisha sheria na utaratibu iliwabidi waweke seng"enge kuyatenganisha makabila mbalimbali. Waliweka mamia ya polisi kuwanyamazisha makutano. Hizo nafsi zenye njaa zilikuwa zimetoka maili nyingi. Malkia mmoja kutoka Rhodesia alikuwa amekuja na gari la moshi lililokuwa na mabehewa 27 yaliyojaa wananchi Waafrika. Walijitahidi kuvuka mashamba na kupanda milima huku wamewabeba migongoni mwao kwa maili kadha wa kadha wapendwa wao waliohitaji msaada. Nchi nzima ilitikiswa na matendo makuu yaliyodhihirishwa na Roho Mtakatifu.

Alasiri moja wakati nilipoanza kuhudumu, mmoja wa maelfu ya Waislamu alikuja jukwaani. Mwanamke huyo aliposimama mbele yangu, mmishenari mmoja kwa Waislamu akaanza kumsihi Bwana kwa utulivu, "Ee, kwa ajili ya nafsi hiyo ya thamani. Loo, kwa ajili ya nafsi hiyo ya thamani." Alikuwa amekaa kule kwa miaka na miaka, na kulingana na ushuhuda wake mwenyewe, alikuwa amepata kuona Mwislamu MMOJA tu akija kumpokea Yesu Kristo kama Mwokozi. Wao kwa asili yao walikuwa Wamedi na Waajemi ambao sheria zao hazibadiliki. Ni wagumu sana kuwapata. Inaonekana kana kwamba "ukisha kuwa Mwislamu daima utakuwa Mwislamu" ndio sheria miongoni mwao.

Vema, wakati alipokuwa amesimama pale mbele zangu, nilianza kuzungumza naye na kwa hao maelfu wote kupitia kwa wakalimani. Nikasema, "Je! sio kweli kwamba wamishenari wamewaambia juu ya YESU aliyekuja kuwaokoa?" Laiti mngaliwaona hao watu wakiangaliana niliposema jambo hilo. Basi walipojibu ya kwamba hiyo ni kweli nikaendelea na kusema, "Lakini je! wamishenari waliwasomea kutoka katika Kitabu hiki (nikainua Biblia yangu juu wapate kuona) ya kwamba Yesu huyu huyu alikuwa mponyaji mwenye nguvu, na ya kwamba Yeye angeishi ndani ya watu Wake katika nyakati zote mpaka atakapokuja tena kuwapokea Kwake Mwenyewe? Je! waliwaambia ya kwamba kwa sababu ya Roho yeye yule ndani yao ambaye alikuwa ndani ya Yesu ya kwamba wao wangeweza kufanya kazi kuu kama vile Yesu alivyofanya? Je! waliwaambia ya kwamba mnaweza kuponywa, kama vile tu mnavyoweza kuokolewa? Ni wangapi wenu wangetaka kumwona Yesu huyu huyu akishuka kati yetu na kutenda mambo yale yale aliyotenda wakati alipokuwa hapa duniani zamani sana?" Wote walitaka jambo hilo. Hilo ni jambo moja ambalo hakika

walikubaliana.

Ndipo nikaendelea, "Kama Yesu kwa Roho Wake atafanya alilofanya alipokuwa duniani, mtaamini Neno Lake, basi?" Na huyu hapa yule mwanamke Mwislamu mbele yangu. Roho akaanza kutenda kazi kupitia kwangu.

Nikamwambia, "Sasa, unajua ya kwamba sikujui. Hata siwezi kuzungumza lugha yako." Alikubali jambo hilo. Nikasema, "Kuhusu kukuponya, unajua siwezi. Lakini ulisikia ule ujumbe alasiri ya leo na ukanielewa." Mkalimani wake wa Kihindi akamjibia ya kwamba alifahamu, kwa maana yeye alikuwa amesoma Agano Jipya.

Sasa Waislamu ni ukoo wa Ibrahimu. Wanamwamini Mungu Mmoja. Lakini wanamkataa Yesu kuwa Mwana wa Mungu na badala yake wanamchukua Mohamedi kama nabii Wake. Wanasema ya kwamba Yesu kamwe hakufa na kafufuka tena. Wao wanafundishwa jambo hilo na masheikh wao nao wanaliamini.

Nikasema, "Lakini Yesu alikufa na akafufuka tena. Yeye alimtuma Roho Wake juu ya kanisa. Roho huyo aliyekuwa ndani Yake ni Roho yeye yule kanisani sasa na anaweza na atazaa kile Yesu alichotoa.

Alisema katika Yohana 5:19,

> *"Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda; kwa maana yote ayatendayo Yeye, ndiyo ayatendayo Mwana vile vile."*

Sasa basi, kama Yesu atakuja na kunifunulia mimi shida yako ni nini, ama sababu yako ya kuja hapa_kama anaweza kuniambia mambo yako yaliyopita, bila shaka unaweza kuamini kwa ajili yale ya usoni?"

Alisema kupitia kwa mfasiri wake, "Naam, ninaweza."

Nikasema, "Vema, na afanye hivyo."

Hao Waislamu walikuwa wakiangalia kwa makini. Wote walikuwa wameinama mbele kuona kitakachotukia.

Ndipo Roho Mtakatifu akanena, "Mume wako ni mtu mfupi, mnene, mwenye sharubu nyeusi. Una watoto wawili. Ulikuwa kwa daktari kama siku tatu zilizopita naye akakufanyia uchunguzi. Una uvimbe kwenye tumbo la uzazi."

Yeye aliinamisha kichwa chake na kusema, "Hiyo ni kweli."

Nikamwuliza, "Kwa nini ukaja kwangu mimi, Mkristo? Kwa nini hukuenda kwa nabii wako wa Kiislamu?"

Akasema, "Nafikiri unaweza kunisaidia."

Nikasema, "Siwezi kukusaidia, lakini kama ukimpokea Yesu Kristo kama Mwokozi wako, Yeye aliye hapa sasa, na anajua yote kukuhusu, Yeye atakusaidia."

Akasema, "Ninamkubali Yesu kama Mwokozi wangu." Hilo lilitosha. Aliponywa na Waislamu wapatao elfu kumi wakamjia Kristo siku hiyo kwa sababu Injili ilihubiriwa kwa Neno na uwezo pia. Mungu hakumwambia mwanadamu ataabike miaka thelathini na asivune kitu. Yeye alitupa mlango uliofunguliwa wa Neno na nguvu na hizo ndizo tunazopaswa kutumia. Hizo ndizo zilizompa Paulo huduma yake kuu na iliyofanikiwa sana. I Wakorintho 2:4, "Na neno langu na kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali kwa dalili za Roho na za nguvu."

Nisikilizeni sasa. Wakati tulipokuwa kwenye ziara hii hii ambapo nilikuwa nikipanda ndege kule New Salisbury, Rhodesia, ndipo ambapo niliona kundi la watu wanne wenye pasipoti za Marekani. Niliwaendea na kusema, "Halo, naona mna pasipoti za Marekani. Mnasafiri kwenda mahali fulani?"

Yule kijana akanijibu, "La, sisi sote ni wamishenari hapa."

"Ni jambo zuri iliyoje," nilimjibu. "Hivi mko peke yenu ama mnafanyia kazi shirika fulani?"

"Sisi ni Wamethodisti. Tunatoka Wilmore, Kentucky," akasema.

"Vema, hapo karibu ni nyuma ya uwanja wangu wa nyuma," nikajibu.

"Wewe siye yule Ndugu Branham ambaye anatokea sehemu hizo?"

Nikasema, "Naam, hiyo ni kweli." Hilo lilimtibu. Asingesema jambo lingine—na jinsi yeye na hao wasichana watatu walivyotazamana. Basi nikasema, "Hebu kidogo mwanangu, ningetaka kuzungumza nanyi nyote kuhusu kanuni fulani, kwa kuwa sisi sote ni Wakristo na tuko hapa kwa ajili ya kusudi kubwa sana. Sasa mnasema nyote wanne mmekuwa hapa miaka miwili. Mnaweza kusema katika Jina la Yesu ya

kwamba mnaweza kunyoshea kidole mtu mmoja ambaye mnajua mmemleta kwa Bwana?" Wasingeweza kufanya hivyo.

"Sitaki kuwaudhi, enyi wasichana," nikasema, "lakini nyote mnapaswa kuwepo nyumbani mkiwasaidia mama zenu kuosha vyombo. Hamna shughuli yo yote huku nje kwenye shughuli za umishenari isipokuwa mmejazwa na Roho Mtakatifu na mnahubiri Injili ya kweli katika dhihirisho la nguvu za Roho Mtakatifu. Kama hamwoni matokeo ambayo Yesu alisema mngeyaona, ni kwa sababu hamhubiri Injili ya kweli."

Hebu nipige hatua moja mbele na niwaonyeshe tu jinsi mambo yanavyoweza kuwa kwenye kazi ya kimishenari. Sisemi ndivyo ilivyo kote, lakini nasikitika sana sana mengi ndivyo yalivyo. Ilikuwa ni wakati nilipokuwa kwenye safari hii hii na nikitembelea karibu na Durban pamoja na meya ambapo nilimwona mwananchi aliyekuwa na kipande kidogo kimefungiwa shingoni mwake naye alikuwa amebeba kinyago. Nikamwuliza rafiki yangu kipande hicho kilikuwa ni cha nini naye akasema ya kwamba wakati mwananchi anapokubali Ukristo wao wanampa kipande. Hilo kwa hakika lilinishangaza, kwa maana hapa pana mtu anayejiita Mkristo, na huku anabeba sanamu hiyo, kwa hiyo nikauliza jambo hilo linawezekanaje.

Akasema, "Ninaweza kuzungumza lugha yake. Hebu na twende tukazungumze naye."

Kwa hiyo tukamwendea na yule meya akawa kama mkalimani wangu. Nilimwuliza mwenyeji kama alikuwa Mkristo. Yeye alithibitisha ya kwamba hakika alikuwa Mkristo. Kisha nikauliza ni kwa nini aliibeba sanamu kama alikuwa Mkristo. Alijibu kwamba ilikuwa sanamu ambayo baba yake alikuwa ameibeba na akamwachia. Nilipomwambia hakuna Mkristo anayepaswa kubeba sanamu alijibu ya kwamba kinyago hiki kilimfaa sana Baba Yake. Nilikuwa na shauku ya kujua ni kwa jinsi gani, naye akasema ya kwamba siku moja baba yake alikuwa ananyemelewa na simba, kwa hiyo akawasha moto na kuongea na kinyago kile jinsi ile alivyokuwa amefundishwa na mchawi. Yule simba akaondoka. Nikamjulisha ya kwamba moto ndio uliomfukuza huyo simba kwa maana moto huwaogopesha wanyama wote wa mwituni. Sitasahau jibu lake kamwe. Akasema, "Vema, ni hivi, kama Amoya (Roho) akishindwa, basi kinyago hiki hakitashindwa." (

(Masimulizi ya kina kuhusu kampeni ya Afrika yanaweza kupatikana katika kitabu, "Nabii Atembelea Afrika.")

Hizo ndizo karibu nguvu zote walizo nazo Wakristo wengi sana kwa sababu Neno halikuletwa kwao kwa ule mlango uliofunguliwa wa hapo asili wa Pentekoste.

Sasa tukirudi kwenye mlango uliofunguliwa wa kimishenari wa Wakati wa Filadelfia. Haukuwa na mlango uliofunguliwa wa nguvu kama ulivyopaswa kuwa nao. Angalia kwenye aya ile ile Yeye anataja mlango huu uliofunguliwa. Yeye anasema, "Una nguvu kidogo." Hiyo ni kweli. NGUVU za Roho hazikuwepo katika wakati huo. Neno lilihubiriwa vizuri. Liliweza vizuri sana kuwafanya watu wawe na hekima kufikia wokovu. Lakini zile nguvu kuu za Mungu ambazo zilionyesha kazi Zake kuu, zilizoungua mkono wake kwa niaba ya walio Wake hazikuwako isipokuwa miongoni mwa makundi yaliyotawanyika. Hata hivyo, Mungu asifiwe, zilikuwa zinakua na ziliongezeka kuzidi zile walizokuwa nazo katika yale matengenezo.

Ni katika wakati huu ambapo yule mtu ambaye mara nyingi tunamwita baba wa misheni alipoingia kazini. William Carey, fundi viatu wa kijijini, aliyekuwa mchungaji wa Kanisa la Kibatisti la Particular huko Moulton, Uingereza, aliwaamsha watu kwa nguvu kuu kwa kuhubiri juu ya, "kama ile amri waliyopewa Mitume ya kufundisha mataifa yote haikuwa ya lazima kwa wahudumu wote hata ukamilifu wa dahari, kwa kuwa ahadi inayoambatana nayo ilikuwa ya kudumu vile vile." Yeye alipigwa vita na Wakalvini ambao walikuwa wamepita mpaka wa fundisho la kuteuliwa wakiamini ya kwamba wote watakaookolewa WATAOKOLEWA na kazi ya umishenari ingekuwa kinyume cha kazi ya Roho. Lakini Andrew Fuller alimsaidia Bw. Carey kwa kuhubiri kwake na kuchangisha pesa. Jitihada yao ilikuwa hivi kwamba shirika liliundwa la kueneza Injili kwa mataifa yote, katika mwaka wa 1792. Shirika hili lilimtuma Carey ambaye alibarikiwa na Mungu sana katika kuwavuta watu huko India. Katika mwaka wa 1795 Ukristo uliopamba moto uliunda Shirika la Kimishenari la London ambalo tunalijua vizuri sana lilichanga mamilioni ya pauni, na kuwatuma maelfu ya wamishenari kwa miaka kadha kutekeleza mapenzi ya Bwana. Roho wa Mungu alikuwa akitenda kazi na "Kondooo Wengine" huenda hata kingekuwa ndicho kilio cha moyoni cha hao waamini wa kweli.

*"Nimekupa mlango uliofunguliwa mbele yako."* Ninataka kuyaangalia maneno haya tena. Wakati huu, ingawa sitayaondoa kwenye umishenari, nitawaletea wazo ambalo linaingia ndani kabisa katika wakati wa mwisho. Kama vile tayari nilivyokwisha sema, wakati huu unatokomea na kuingia katika wakati wa mwisho. Ni katika wakati huu ambapo Yesu alisema, "Naja upesi" (aya ya 11), na kuhusu wakati wa mwisho Yeye alikuwa anaenda "kuimaliza kazi na kuikata katika haki; kwa maana Bwana atafanya kazi ya kumaliza upesi juu ya nchi." Warumi 9:28. Angalia jinsi aya hii ya Ufunuo 3:8 inavyoenda_"mlango uliofunguliwa_nguvu kidogo, Neno, Jina." Mlango huo uliofunguliwa una uhusiano na yote matatu. Sasa mlango unamaanisha nini?

Katika Yohana 10:7, inasema,

*"Basi Yesu aliwaambia tena, Amin, amin, nawaambieni, MIMI NDIMI MLANGO WA*

*KONDOO."*

Hiyo ni kweli: 'MIMI NIKO' ni mlango wa kondoo. Sasa haya si maneno ya kushangaza tu. Hii ndivyo ilivyo hasa. Angalia katika Yohana 10 wakati Yesu anapotoa mfano huu, Yeye Mwenyewe anajiita ni yule mchungaji. Kisha anajiita Mwenyewe ni ule mlango. Na hivyo ndivyo mchungaji alivyo kwa kondoo. Yeye kwa kweli ndiye mlango wao.

Nilipokuwa kule Mashariki niliona ya kwamba wakati wa usiku mchungaji angewakusanya kondoo wake wote pamoja. Atawaingiza katika zizi. Kisha angewahesabu. Alipohakikisha ya kwamba wote wameingia, atalala chini kwenye mlango uliofunguliwa wa hilo zizi na awe kweli ni mlango wa kuingilia zizini. Hakuna mtu angeweza kuingia wala kutoka ila kwa yeye. Yeye alikuwa mlango. Kesho yake nilipokuwa kwenye gari la aina ya jip pamoja na rafiki yangu, niliona ya kwamba mchungaji mmoja alianza kuongoza kundi lake kuelekea mjini. Mara moja magari yote yakasimama ili kwamba wale kondoo wapite. Sasa miji kule Mashariki si kama ilivyo hapa. Sisi tunaweka bidhaa zetu zote ndani; lakini kule, ni kama soko kubwa la wakulima ikiwa mazao yote yamewekwa kando ya barabara kusudi watu wanaopita wayaone na kuyanunua. Nikawaza, "Loo jamani, hapa ndipo ghasia zinaanza. Ngojeni mpaka hao kondoo watakapoona chakula hicho chote kule." Lakini wakati mchungaji aliposonga mbele, hao kondoo walifuata moja kwa moja kabisa katika kila hatua. Wangeangalia mambo hayo yote mazuri, bali hakuna kondoo aliyegusa kitu. Loo! laiti tu ningalijua lugha yao, ningalisimamisha hayo magari mimi mwenyewe na kuwahubiria mahubiri juu ya yale niliyoyaona punde.

Wakati wewe ni kondoo wa yule Mchungaji Mkuu, unafuata moja kwa moja katika kila moja ya hatua Zake, kama tu vile hao kondoo walivyofanya. Hutashawishiwa kugeukia kando kwa ajili ya ua fulani kubwa la kanisa fulani, ama kusikiliza sauti ya D.D. fulani ama Ph.D. ama L.L.D., lakini utakaa pamoja na yule Mchungaji. Biblia inasema ya kwamba kondoo wanaijua sauti Yake nao wanamfuata YEYE, lakini sauti ya mgeni itawafanya tu kutoroka na kumkimbilia Mchungaji wao wa kweli. Mungu asifiwe.

Lakini si hayo tu niliyoona na kujifunza kule. Siku moja nilianza kufikiria juu ya kuwaona watu kondeni wakichunga wanyama wa aina mbalimbali. Mtu mmoja angekuwa akichunga nguruwe, mwingine mbuzi, mwingine ngamia, mwingine nyumbu, na kadhalika. Kwa hiyo nikamwuliza rafiki aliyeishi pale, kile walichowaita hao watu. "Loo," akajibu, "hao ni wachungaji."

Singeweza kuamini jambo hilo. Nikasema, "Humaanishi ya kwamba hao WOTE ni wachungaji. Wachungaji huwachunga kondoo tu, sivyo?"

"La," akasema, "mchungaji ni mwenye kuchunga au kulisha, kwa hiyo mtu ye yote anayewalisha wanyama ni mchungaji."

Vema, hilo lilinishangaza. Lakini niliona tofauti kati ya hao wachungaji na wale waliowachunga kondoo. Usiku ulipoingia hao wengine wote isipokuwa wachungaji wa kondoo waliwaacha wanyama wao makondeni wakaenda zao nyumbani. Yule mchungaji aliondoka pamoja na kondoo zake, na kuwaingiza zizini kisha alilala chini na akawa mlango wa kondoo. Loo! Mungu asifiwe, Mchungaji wetu hatuachi kamwe wala kutupungukia. Wakati usiku unapoingia ninataka kuwa katika zizi Lake. Ninataka kuwa katika ulinzi Wake.

Sasa basi, tunaweza kuona ya kwamba YESU NDIYE MLANGO. Yeye ni mlango wa kondoo. Na angalia ya kwamba inasema sasa kuhusu MLANGO KUFUNGULIWA. Ni kitu gani hicho ila ufunuo Wake? Na huo ufunuo unafunguka upate kutuletea Nguvu, kuliangazia Neno na kulitukuza Jina Lake. Ilikuwa katikati ya zile nyakati mbili za mwisho ambapo Ufunuo wa Uungu wa Yesu Kristo ulichanua mbele zetu. Naam, tulijua Yeye alikuwa ni Mungu. Angewezaje kuwa Mwokozi wetu? Lakini kujua ya kwamba YEYE ALIKUWA MUNGU TU, AMA MUNGU PEKEE, ya kwamba alikuwa Alfa na yule Omega, ya kwamba "Yesu huyu alikuwa BWANA NA KRISTO PIA—KIMFANYA BWANA YESU KRISTO, BABA, MWANA NA ROHO MTAKATIFU, YOTE MTU MMOJA—hilo lilikuwa limepotea tangu nyakati za kwanza za kanisa, lakini sasa tunaliona tena. Ufunuo wa YEYE ALIKUWA NI NANI ulikwisha kurudi. Kweli Uungu si Mungu wa watu watatu walio na nafsi moja, kwa maana inahitaji utu kumfanya nafsi. Kama kuna utu Mmoja, kuna mtu mmoja tu. Lakini hao wanaoamini katika nafsi tatu wana Uungu wa miungu watatu nao wana hatia ya kuvunja amri ya kwanza.

Lakini ufunuo wa Uungu umerudi. Sasa kanisa la kweli linaweza kujenga katika nguvu tena. Baada ya wakati huu wote hatimaye linajua Bwana wake ni Nani. Mara nyingine tena TUNABATIZA KATIKA JINA LA BWANA YESU kama tu walivyofanya wakati wa Pentekoste.

Hebu niwaambie juu ya ndoto niliyopewa na Mungu niliyoota kuhusu ubatizo wa utatu. Hili halikuwa ni ono, bali ni ndoto. Mnajua, nina hakika, ya kwamba moja ya baraka za nyakati za kanisa ilikuwa ni kupokea ndoto kwa Roho Mtakatifu, kama vile vile tu mtu anavyoweza kupokea maono. Ilikuwa usiku kuamkia Jumamosi kama saa 9 usiku. Nilikuwa ndiyo tu nimeamka ili kumpa Joseph maji ya kunywa. Nilipolala nilishikwa na usingizi mara moja na kuota ndoto hii. Nilimwona mtu ambaye nilidhani alikuwa ni baba yangu. Alikuwa ni mtu mkubwa mno na mnene. Pia niliona mwanamke aliyedhaniwa kuwa ni mama yangu, lakini hakufanana naye, kama vile mwanamume huyo asivyokuwa anafanana na baba yangu. Mtu

huyu alikuwa ni mbaya sana kwa mkewe. Alikuwa na rungu kubwa lenye pembe tatu juu yake. Unajua unapochukua gogo na kulilaza chini na kulipasua upande mmoja mwishoni kwa shoka, linatoa ukuni wenye sehemu tatu kama kabari. Lilikuwa namna hiyo. Yeye angechukua rungu hii na kumpiga nayo, na kumbwaga chini. Akiwa amelala hapo analia, angetembea huku na huko kifua mbele na usoni mwake mlikuweko na kiburi na majivuno hivi kwamba alionekana anaona fahari na kuridhika kwa kumpiga maskini mwanamke yule mdogo. Kila wakati alipojaribu kuinuka yeye angempiga kumbo. Sikupendezewa na alilokuwa anafanya, lakini nilipokuwa ninawazia juu ya kumkomesha, niliwaza, "Siwezi kumdhibiti mtu yule_yeye ni mkubwa kupita kiasi. Ndipo anapaswa kuwa baba yangu." Lakini ndani moyoni nilijua yeye hakuwa baba yangu, na nilijua ya kwamba hapana mtu aliye na haki ya kumtendea mwanamke namna hiyo. Nikaondoka nikaenda nikamshika kwa nguvu kwenye ukosi na kumgeuza nikasema, "Huna haki ya kumpiga." Na niliposema jambo hilo misuli yangu ilikua nami nikaonekana kama lijitu likubwa. Mtu huyo akaiona na ndipo akaniogopa. Nikasema, "Mpige tena nawe utapambana nami." Alisita kumpiga tena, ndipo ndoto ikaniacha.

Niliamka mara baada ya ile ndoto. Nikawaza, jinsi hilo lilivyokuwa la ajabu. Sikujua ni kwa nini niliota juu ya mwanamke huyo, ndipo mara Huyo hapo Yeye akaja, na uwepo wa Mungu ukajulikana kwangu na tafsiri ya hiyo ndoto ikatoka Kwake. (Sasa ninyi watu mnajua ya kwamba si kwamba tu nimewafasiria ndoto zenu sawa sawa kabisa; lakini nimewaambia mara nyingi, nyingi sana, yale mliyoota hivi kwamba haikuwabidi ninyi kuniambia.) Mwanamke anawakilisha kanisa la ulimwengu leo. Nilizaliwa moja kwa moja katika machafuko haya—machafuko aliyomo. Alipaswa kuwa mama wa namna fulani (yeye ni mama wa makahaba). Mumewe ndiye madhehebu yanayomtawala. Lile gogo lenye pembe tatu ni ubatizo wa uongo wa nafsi tatu katika utatu wa miungu. Kila wakati alipoanza kuinuka (hiyo inamaanisha kusanyiko lilipoanza kukubali ukweli) yeye angemtwanga chini tena moja kwa moja kwa fundisho hilo la uongo. Alikuwa mkubwa sana hata nilimwogopa mara ya kwanza, lakini nilipomkabili nilikuta kwamba nilikuwa na misuli mikubwa na yenye nguvu. Ilikuwa ni MISULI YA IMANI. Matokeo ya ndoto hiyo ilikuwa kwamba, "kwa kuwa Mungu yu pamoja nami, na anaweza kunipa nguvu kama hizo, basi hebu nimpiganie dhidi ya nguvu za kimadhehebu za ulimwengu na kumkomesha aache kumpiga."

Sasa mimi sijaribu kujenga fundisho juu ya ndoto. Wala sijaribu kuthibitisha fundisho lo lote ninalotetea kwa ndoto. Umoja wa Uungu uko kote tangu Mwanzo 1:1 hadi Ufunuo 22:21. Lakini watu wamepofushwa na fundisho la sharti lisilo la kimaandiko la utatu, na fundisho hilo la sharti limekubalika sana duniani kote hivi kwamba kujaribu kuona "Mungu Mmoja wa Nafsi Moja" haiwezekani kabisa. Kama watu hawawezi daima kuona KWELI ya Uungu, bali wanaipinga; hawataweza sikuzote kuona kweli nyingine kwa sababu UFUNUO NI YESU KRISTO KATIKA KANISA LAKE NA KAZI ZAKE KATIKATI YA KANISA KWA ZILE NYAKATI SABA. Umeliona jambo hilo? Sasa nina hakika mnaelewa.

*"Unazo nguvu kidogo, nawe umelitunza Neno Langu, wala hukulikana Jina Langu."* Sasa tayari tumeishasema ni jinsi gani nguvu zile zilivyokuwa zikirudi. Zilikuwa zinarudi. Nguvu za baraza kuu la kuhukumu wazushi wa dini zilikuwa zimefifia. Watu walikuwa wameondoka kwenye nchi za uenyeji wao na kudai uhuru wa kuabudu. Nira ya serikali ya ukasisi ilikuwa inavunjwa. Serikali zilikuwa zilikuwa zikiona ni jambo la busara kutounga mkono kundi moja dhidi ya jingine. Kwa kweli, watu wenye nia nzuri lakini walioongozwa vibaya walikuwa tayari kupigana vita kusudi watetee haki zao za kidini. Labda onyesho kubwa sana la nguvu za kidini katika wakati huu lilikuwa ni ukweli, ya kwamba ingawa Ufaransa iliangushwa katika mapinduzi, ule ufufuo mkuu wa Kiwesley ulizuia mapinduzi yasiingie Uingereza na ukaiokoa ipate kuwa chombo katika mkono wa Mungu kwa miaka mingi yenye fahari.

Kuhubiriwa kwa Neno hakukuongezeka hata kidogo. Wakati shetani alipokuwa akiinua makundi yake ya maharamia wenye mawazo huru, waanzilishi wa ukomunisti walipoinuka, wanatheolojia wa kimapinduzi walipokuwa wakieneza bidhaa zao chafu, Mungu aliinua mashujaa hodari wa imani, na vitabu muhimu sana vya Kikristo na mafundisho na mahubiri vilitokea katika kipindi hiki. Kamwe hakujatokea na hakutatokea wahubiri na waalimu kama wake. Akina Spurgeon, Parka, Meklaren, akina Edward, Bunyan, Meula, Brainard, Barne, Bishop, wote walitokea kwenye kipindi hiki. Walihubiri, walifundisha na kuandika Neno. Walilitukuza Jina Lake. HUKUMU YA WAYAHUDI WA UONGO

**HUKUMU YA WAYAHUDI WA UONGO**

Ufunuo 3:9.

> *"Tazama, nakupa walio wa sinagogi la Shetani, wasemao kwamba ni Wayahudi, nao sio, bali wasema uongo; tazama, nitawafanya waje kusujudu mbele ya miguu yako, na kujua ya kuwa nimekupenda."*

Sasa tunaweza kuona mara moja ya kwamba tatizo hili la Wayahudi wa uongo ama waamini wa uongo lilikuweko tayari katika wakati wa pili. Hawa ambao walijiita Wayahudi kwa uongo walitokea mara baada ya kumwagika kwa wingi kwa kwanza kwa ule wakati wa kwanza, na sasa wanatokea tena katika wakati wa pili baada ya yale matengenezo. Hii ni kwa bahati mbaya. Hakika, si kwa bahati mbaya. Ni kanuni ya Shetani. Kanuni hiyo ni kuunda madhehebu na kudai kuwa ndio waanzilishi na hivyo basi

kustahili haki na heshima maalum. Hebu niwaonyeshe. Huko nyuma katika Wakati wa Smirna watu hawa walidanganya na kusema wao kweli walikuwa ni Wayahudi (ama waamini) wakati hawakuwa hivyo kabisa. Walikuwa wa sinagogi la Shetani. Wao walikuwa kundi la Shetani lililounda madhehebu, kwa kuwa ilikuwa ni katika wakati huo tulipoona mwanzo wa watu katika huduma wakichukua uongozi usio wa haki juu ya ndugu zao wanaohudumu. (Maaskofu wamewekwa katika wilaya, juu ya wazee). Jambo la pili tuliloona ni kwamba katika wakati wa tatu hakika kulikuwa na mahali panapoitwa "kiti cha Shetani". Wakati huo ulitupa ndoa ya kanisa na serikali. Huku nguvu za serikali zikiwa nyuma yake kanisa lilikuwa kimwili haliwezekani kabisa.

Lakini Mungu aliivunja ngome hiyo bila kujali nguvu za serikali na matengenezo yakaleta nuru kuu. Lakini ni jambo gani lililotukia? Waluteri waliunda dhehebu na kujiunga na serikali na ndipo tena tunaona sinagogi la Shetani likidhihirishwa katika wakati huu wa sita. Sasa bila shaka kundi hili la sinagogi halingesema ni la Shetani. La bwana. Wanasema wao ni wa Mungu. Lakini wao wanasema uongo. Kwa kuwa Yeye aliye Myahudi wa kweli (hivyo ndivyo walivyodai kuwa) ni yule aliye Myahudi kwa ndani—katika Roho. Kwa hiyo kama wao ni Wayahudi wa uongo inamaanisha wao ni kama vile Yuda 19 inavyosema, "WASIO na Roho." Watoto wa Mungu wamezaliwa kwa Roho. Hawa hawana Roho na kwa hiyo wao SI wana wa Mungu haidhuru wakatae kwa nguvu namna gani na waende umbali gani kujaribu kuthibitisha ya kwamba wao ni watoto wa Mungu. Wao WAMEKUFA. Wao ni watoto wa madhehebu, na matunda ya kweli hayapo. Wamejengwa juu ya kanuni zao wenyewe, mafundisho ya sharti na mafundisho ya dini wala kweli haimo ndani mwao kwa maana wao wameweka mashauri yao yawe juu ya Neno la Mungu.

Hebu niwaonyeshe jambo ambalo nimekuwa nikijaribu kufundisha wakati wote kuhusu ile mizabibu miwili inayotokana na roho mbili tofauti. Chukua mfano wa Yesu na Yuda wakati huu. Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Yuda alikuwa mwana wa upotevu. Mungu aliingia ndani ya Yesu. Shetani aliingia kwa Yuda.

Yesu alikuwa na huduma kamili ya Roho Mtakatifu

> *"Jinsi Mungu alivyomtia Yesu wa Nazareti mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu; Naye akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na Ibilisi; kwa maana Mungu alikuwa pamoja Naye."*

Matendo 10:38. Inasema

> *"Kwa yeye (Yuda) alikuwa amehesabiwa pamoja na sisi, akapata SEHEMU ya huduma hii,"*

Matendo 1:17. Mathayo 10:1,

> *"Akawaita wanafunzi Wake kumi na wawili, akawapa amri juu ya pepo wachafu, wawatoe, na kupoza magonjwa yote na udhaifu wa kila aina."*

Roho yule aliyekuwa ndani ya Yuda alienda moja kwa moja kupitia katika huduma ya Yesu. Ndipo wote wawili wakaja msalabani. Yesu alisulibishwa msalabani, akiutoa Uhai Wake kwa moyo kwa ajili ya wenye dhambi na kuiweka Roho Yake kwa Mungu. Roho Yake ilienda kwa Mungu kisha ikamwagwa ndani ya kanisa wakati wa Pentekoste. Lakini Yuda alijinyonga na roho yake ikamrudia Shetani, lakini baada ya Pentekoste roho yuyo huyo aliyekuwa ndani ya Yuda alirudi mzabibu wa uongo ambao unakua moja kwa moja pamoja na mzabibu wa kweli. Lakini angalia, roho ya Yuda haikufika kwenye Pentekoste. Haikuendelea hata impokee Roho Mtakatifu. Haikuweza. Isingeweza. Lakini hiyo roho ya Yuda ilikusudia nini? Ilifuatilia mfuko wa dhahabu. Jinsi ilivyopenda pesa. Bado inapenda pesa. Kama inakwenda huku na huko kwa Jina la Yesu ikitenda mambo makuu na kuendesha mikutano mikubwa, bado ingali inatengeneza pesa zaidi na kujenga majumba zaidi, na elimu na kila kitu ikiwa na wazo la mali. Angalia tu huyo roho aliye juu yao na usipumbazwe. Yuda alienda kama mmoja wa wale kumi na wawili naye alifanya miujiza, pia. Lakini Yeye HAKUWA na Roho wa Mungu kama wake binafsi. Yeye kweli alikuwa na huduma fulani. Hakufikia Pentekoste kamwe kwa maana hakuwa mzao wa kweli. Yeye hakuwa mtoto wa kweli wa Mungu. La bwana. Na ndivyo ilivyo sasa hivi katika sinagogi la Shetani. Msidanganywe. Hutadanganywa kama wewe ni mmoja wa wateule. Yesu alisema hamtadanganywa.

Naam, hawa watu wanasema wao ni Wakristo lakini si Wakristo.

*"Nitawafanya waje kusujudu mbele ya miguu yako, na kujua ya kuwa nimekupenda."*

I Wakorintho 6:2,

> *"Au hamjui ya kwamba Watakatifu watauhukumu ulimwengu?"*

Hakutakuwapo na wale mitume kumi na wawili tu kwenye viti kumi na viwili wakiyahukumu yale makabila kumi na mawili ya Israeli bali na watakatifu, pia, watauhukumu ulimwengu. Hapo ndipo hawa wanaodai kwamba ni wa Mungu na kudai ya kwamba Mungu anawapenda watakapopata kujua hakika

kabisa mtoto wa Mungu ni nani na ni nani anayependwa na Mwana. Naam, siku hiyo inakuja ambapo itadhihirishwa. Hawa ambao sasa wanautawala ulimwengu kwa kiasi fulani, na ambao katika wakati ule wa mwisho watatengeneza sanamu ya mnyama ambapo kwa kweli watautawala ulimwengu, siku moja wataaibishwa wakati Yesu atakapokuja pamoja na watakatifu Wake kuuhukumu ulimwengu katika haki. Hilo ndilo tuliloona hasa katika Mat. 25 wakati "Wote" wale wasiokuwemo katika ufufuo wa kwanza watakaposimama mbele ya Hakimu na bibi-arusi Wake.

**SIFA NA AHADI**

Ufunuo 3:10,

> *"Kwa kuwa umelishika Neno la subira Yangu, mimi nami nitakulinda, utoke katika saa ya kujaribiwa iliyo tayari kuujilia ulimwengu wote, kuwajaribu wao wakaao juu ya nchi."*

Yeye anamaanisha nini kwa kusema "neno la subira Yake?" Waebrania 6:13- 15. *"Kwa maana Mungu, alipompa Ibrahimu ahadi, kwa sababu alikuwa hana mkubwa kuliko Yeye Mwenyewe wa kumwapa, aliapa kwa nafsi Yake, akisema, Hakika Yangu kubariki nitakubariki, na kuongeza nitakuongeza. Na hivyo kwa kuvumilia akaipata ile ahadi."* Mnaona Roho anazungumza juu ya Neno la Mungu ambalo tumepewa. Kule kungojea kule kutimizwa kwa Neno hilo kulihitaji subira kama tu ilivyokuwa kwa Ibrahimu. Alivumilia kama kwamba alimwona Yeye asiyeonekana. Yeye alikuwa na saburi na halafu hatimaye Neno lilitimizwa. Hivi ndivyo Mungu anavyowafundisha watu Wake saburi. Mbona, kama Yeye angalilitimiza Neno Lake katika madhihirisho ya maumbile papo hapo ulipoomba, hungeweza kujua subira ni nini hata kidogo, lakini ungekuwa hata zaidi na zaidi mtu asiye na subira na maisha. Hebu niwaoneshe kweli hii iliyooneshwa kikamilifu zaidi.

Waebrania 11:17,

> *"Kwa imani Ibrahimu, alipojaribiwa, akamtoa Isaka awe dhabihu; na yeye aliyezipokea hizo ahadi (Neno la Mungu) alikuwa akimtoa mwanawe, mzaliwa wa pekee."*

Hivyo ndivyo ilivyo: Ibrahimu alijaribiwa BAADA ya kupokea Neno la Ahadi. Watu walio wengi hufikiri ya kwamba mara tu baada ya sisi kuomba katika Jina la Yesu kuhusu ahadi nzuri za Mungu ya kwamba hakungeweza kuwepo na majaribu. Lakini hapa inasema ya kwamba Ibrahimu alijaribiwa baada ya kuipokea ile ahadi.

Hilo ni sahihi kabisa kulingana na Mwandishi wa Zaburi akimzungumza Yusufu, 105:19,

> *"Hata wakati wa kuwadia neno lake, Neno la Bwana lilimjaribu."*

Mungu hutupa ahadi kubwa mno na za thamani. Yeye ameahidi kuzitimiza. Atazitimiza. Lakini tangu wakati tunapoomba mpaka wakati tunapopata jibu hatuna budi kujifunza subira nafsini mwetu kwa maana ni katika subira tu ndipo ambapo tunapokea uzima. Mungu na atusaidie kujifunza somo hili kama vile tunavyojua watu wa wakati huu wa sita walivyojifunza subira. Tunasoma historia ya maisha ya Wakristo hawa mashuhuri; ni tofauti gani tunayoona kati ya maisha yao na yetu kwa maana walikuwa na subira sana na walikuwa watulivu, na leo tumeshindwa katika kukosa subira kabisa na kuwa na haraka.

*Yeye anaendelea kuwaambia, "Kwa kuwa umelichukua Neno Langu na kuliishi na kwa njia hiyo mkawa na subira, nitakulinda na saa ya kujaribiwa itakayoujilia ulimwengu, kuwajaribu wakaao juu ya nchi."* Sasa hapa tena tunaona kule kuingiliana kwa zile nyakati mbili; kwa maana ahadi hii ina uhusiano na mwisho wa wakati wa Mataifa ambao unaishia katika ile Dhiki iliyo Kuu.

*"Nitakulinda, utoke katika saa ya kujaribiwa iliyo tayari kuujilia ulimwengu wote, kuwajaribu wakaao juu ya nchi."* Aya hii si tangazo la kwamba kanisa la kweli litaingia na kupitia katika ile dhiki. Kama ingalimaanisha hilo ingesema hivyo. Lakini ilisema, *"Nitakulinda utoke katika saa ya kujaribiwa."* Jaribu hili ni kama lile kabisa lililokuwa Edeni. Litakuwa ni maneno ya kuvutia sana ambayo yatatolewa kinyume kabisa na Neno la Mungu lililoamriwa, na hata hivyo kwa msimamo wa akili za kibinadamu litaonekana kuwa ni jambo sahihi kabisa, litoalo mwanga sana na kutoa uzima hata linaweza kuupumbaza ulimwengu.

Walio wateule ndio tu hawatapumbazwa. Jaribu litakuja kama ifuatavyo. Zile pilikapilika za ekumeni ambazo zimeanza katika kitu kinachoonekana kama kanuni nzuri sana na yenye baraka (kuyatimiza maombi ya Kristo ya kwamba sote tupate kuwa kitu kimoja) zinapata nguvu sana kisiasa hata zitaishurutisha serikali kuwafanya wote waungane nao aidha moja kwa moja ama kwa kufuata kanuni zilizofanywa sheria hivi kwamba hakuna watu watakaotambuliwa kama makanisa halisi isipokuwa chini ya uongozi wa moja kwa moja ama usio wa moja kwa moja wa halmashauri hii. Makundi madogo madogo yatapoteza mikataba, haki, nk., mpaka watakapopoteza mali yote na haki za kiroho kwa watu.

Kwa mfano, sasa hivi isipokuwa shirika la wahudumu la mtaa fulani likubali katika miji mingi, kama si karibuni yote, mtu hawezi kukodisha jengo kwa ajili ya ibada za dini. Kuwa makasisi jeshini, kwenye mahospitali, nk., sasa hivi karibu ni jambo la lazima kutambuliwa kama mtu ambaye anakubalika na

makundi ya utatu ya ekumeni. Wakati mbano huu unapoongezeka, na utaongezeka, itakuwa ni vigumu zaidi kuupinga, kwa maana kuupinga ni kupoteza haki. Na wengi sana watashawishika kukubaliana nao, kwa sababu wataona ni afadhali kumtumikia Mungu hadharani katika utaratibu uliowekwa na shirika hili kuliko kutomtumikia Mungu hadharani kabisa. Lakini wanakosea. Kuamini uongo wa ibilisi ni kumtumikia Shetani, ingawa unaweza kutaka kumwita Yeye Yehova. Bali wateule hawatadanganywa.

Zaidi ya hayo, wateule si kwamba tu watahifadhiwa, lakini wakati pilikapilika hizi zinapofanyika "SANAMU ILIYOFANYIWA YULE MNYAMA," watakatifu watakuwa wamenyakuliwa. Na shirika hili dogo linalopendeza, linalofurahisha sana lililoanza kule Efeso katika ushirika litakuwa dubwana la Shetani linalonajisi na kuudanganya ulimwengu wote. Kwa maana utaratibu wa kanisa wa Katoliki ya Kirumi na wa Kiprotestanti katika kuungana utamiliki mpango mzima wa mali yote ya ulimwengu na kuishurutisha dunia nzima kuingia katika mtego wake wa kidini, la sivyo utawaua, kwa kuwanyima haki ya kununua na kuuza ambayo kwayo wangejipatia riziki. Jambo hili litatimizwa kwa kirahisi, kwa maana binti wa kahaba karibu wote wamerudi kwake. Wakati huo huo, Rumi imemiliki karibu akiba yote ya dhahabu. Wayahudi wana zile hati za dhamana na noti zote. Katika wakati unaofaa, yule kahaba ataangamiza utaratibu wa sasa wa pesa kwa kuagiza hati zote za malipo zilipiwe, na kudai dhahabu. Bila dhahabu, huo utaratibu unaanguka. Wayahudi wataingia mtegoni na kufanya mapatano, ndipo kanisa hilo la kahaba litauteka uliwengu mzima.

**AHADI KWA WALIO WAKE**

Ufunuo 3:11-12,

*"Tazama, Naja upesi. Shika sana ulicho nacho, asije mtu akaitwaa taji yako.*

*Yeye ashindaye, nitamfanya kuwa nguzo katika hekalu la Mungu Wangu, wala hatatoka humo tena kabisa, nami nitaandika juu yake Jina la Mungu Wangu, na jina la mji wa Mungu Wangu, huo Yerusalemu mpya, ushukao kutoka mbinguni kwa Mungu Wangu, na Jina Langu Mwenyewe, lile jipya.*

Hatuhitaji kutoa maoni juu ya wazo kwamba Yeye yuaja upesi. Tunajua ya kwamba Yeye ni kwa sababu tuko katika mwisho wa siku za mwisho, sivyo? Lakini Yeye anaendelea kusema, "Shika sana ulicho nacho, asije mtu akaitwaa taji yako."

Ni katikati ya wakati wa shida kuu ndipo Yesu anakuja. Na kwa kuja Kwake kuna ufufuo. Wengi watatoka mavumbini na kufufuka pamoja na wale walio hai lakini wakingojea kurudi Kwake. Na hawa watapewa taji. Kwa nini? Kwa sababu wao ni Wana wa Mungu. Wao ni wafalme pamoja Naye. Wanatawala pamoja Naye. Taji inamaanisha hilo—kumiliki na kutawala pamoja na Mfalme Mkuu, Mwenyewe. Hiyo ndiyo ahadi kwa wale wote wanaoteseka pamoja Naye hapa duniani_ hao wote waliovumilia kwa subira wakijua ya kwamba Mungu, yule Hakimu Mwenye Haki atawajazi. Wao waliotoa yote kwa ajili Yake na kuweka yote Kwake wataketi katika kiti Chake cha enzi na kushiriki ufalme Wake wenye utukufu.

Loo, tuna neno kwa ajili yetu sote wakati huu. Ni kushikilia sana—kuvumilia. Usikate tamaa. Vaa silaha zote za Mungu_tumia kila silaha aliyotupa_tumia kila karama tuliyopewa kutumia na tuangalie mbele kwa furaha, kwa sababu tutatiwa taji Naye Ambaye ni Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana.

Sasa Yeye hatoi taji tu lakini anasema ya kwamba hawa walio katika bibi-arusi watafanywa nguzo katika hekalu la Mungu. Lakini hekalu la Mungu ni nini? Yesu alinena juu ya mwili Wake kama hekalu. Ndivyo ulivyokuwa. Lilikuwa ni hekalu la Mungu. Lakini sasa kwa kuwa sisi ni mwili Wake, kanisa la kweli ni hekalu la Mungu kwa Roho Mtakatifu aliye ndani yetu. Sasa Yeye atamfanya mshindi kuwa nguzo katika hekalu hilo. Lakini nguzo ni nini? Nguzo kwa kweli ni sehemu ya msingi kwa kuwa inashikilia sehemu ya juu. Mungu asifiwe, hilo linamweka mshindi moja kwa moja pamoja na mitume na manabii, kwa maana inasema katika Waefeso 2:19-22,

*"Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani Mwake Mungu.*

*Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, Naye Kristo Yesu Mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni.*

*Katika Yeye jengo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana. Katika Yeye ninyi nanyi mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho."*

Naam, kifungu cha 22 kinasema ya kwamba tumejengwa pamoja nao. Kila kitu kilipitia MLANGONI (Yesu) na ni sehemu ya mwili huo ama hekalu. Sasa wakati Mungu anapomweka mtu katika hekalu kama nguzo na kumfanya sehemu ya kundi hilo la msingi Yeye anafanya nini? Yeye anampa ufunuo wa Neno na wa Yeye Mwenyewe, kwa maana huo ndio mitume na manabii waliokuwa nao. Mathayo 16:17. Huyo hapo katika Neno hilo. Huyo hapo amesimama. Hakuna mtu anayeweza kumtoa.

Tafakari neno hilo, “kushinda”. Yohana anauliza swali, “Ni nani yeye ashindaye?” na jibu linarudi moja kwa moja, “Yeye aaminiye ya kwamba Yesu ni Kristo.” Yeye hasemi ya kwamba mshindi ni yule aaminiye katika Yesu „Fulani“ na katika Kristo „Fulani,“ lakini aaminiye ya kwamba Yesu NDIYE KRISTO_mtu MMOJA_si wawili. Huyo ni yule ambaye amebatizwa katika Jina la Bwana Yesu Kristo.

Mungu anazungumza juu ya bibi-arusi hapa. Je! Mnataka kuona picha yake nyingine?

Ni katika Ufunuo 7:4-17,

> *"Nikasikia hesabu yao waliotiwa muhuri katika kila kabila ya Waisraeli, watu mia na arobaini na nne elfu. Wa kabila ya Yuda kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri.*
>
> *Wa kabila ya Reubeni kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. Wa kabila ya Gadi kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri.*
>
> *Wa kabila ya Asheri kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. Wa kabila ya Naftali kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. Wa kabila ya Manase kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri.*
>
> *Wa kabila ya Simeoni kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. Wa kabila ya Lawi kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. Wa kabila ya Isakari kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri.*
>
> *Wa kabila ya Zabuloni kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. Wa kabila ya Yusufu kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri. Wa kabila ya Benyamini kumi na mbili elfu waliotiwa muhuri.*
>
> *Baada ya hayo nikaona, na tazama, mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha, wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi, na mbele za Mwana- Kondoo, wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mitende mikononi mwao;*
>
> *Wakilia kwa sauti kuu wakisema, Wokovu una Mungu wetu aketiye katika kiti cha enzi, na Mwana- Kondoo.*
>
> *Na malaika wote walikuwa wakisimama pande zote za kile kiti cha enzi, na za hao wazee, na za wale wenye uhai wanne, nao wakaanguka kifulifuli mbele ya kile kiti cha enzi, wakamsujudu Mungu,*
>
> *Wakisema, Amina; Baraka na utukufu na hekima na shukrani na heshima na uweza na nguvu zina Mungu wetu hata milele na milele. Amina.*
>
> *Akajibu mmoja wa wale wazee akiniambia, Je! Watu hawa waliovikwa mavazi meupe ni akina nani? Nao wametoka wapi?*
>
> *Nikamwambia, Bwana wangu, wajua wewe. Akaniambia, Hao ndio wanatoka katika dhiki ile iliyo kuu, nao wamefua mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo.*
>
> *Kwa hiyo wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, nao wanamtumikia mchana na usiku katika hekalu Lake, na Yeye aketiye katika kiti cha enzi atatanda hema Yake juu yao.*
>
> *Hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena, wala jua halitawapiga, wala hari iliyo yote.*
>
> *Kwa maana huyo Mwana-Kondoo, aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga, Naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai, na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao."*

Yesu amekuja. Yeye ametia muhuri wale 144,000. Alichukua 12,000 kutoka kila kabila. Lakini kuna kundi lingine ambalo si la hawa 144,000 ambao wanaonekana katika aya ya 9-18. Hao ni akina nani? Hawa ni katika bibi-arusi aliyechukuliwa kutoka miongoni mwa Mataifa. Wako mbele ya kiti Chake cha enzi mchana na usiku. Wanamtumikia hekaluni. Wao wako chini ya ulinzi maalum wa Bwana. Wao ni bibi-arusi Wake.

Bibi-arusi huenda popote alipo Bwana Arusi. Yeye hataachwa Naye kamwe. Yeye hataondoka ubavuni Mwake. Atashiriki kiti cha enzi pamoja Naye. Atatiwa taji kwa utukufu na sifa Zake.

*"Nami nitaandika juu yake Jina la Mungu Wangu, na Jina la mji wa Mungu Wangu.* Na Jina la Mungu ni lipi? Vema, Yeye alikuwa Mungu pamoja nasi, ama Imanueli, lakini hilo halikuwa jina Lake alilopewa. "Utamwita Jina Lake Yesu." Yesu alisema, "Nilikuja katika Jina la Baba Yangu, wala hamkunipokea." Kwa hiyo Jina la Mungu ni YESU, kwa maana hilo ndilo Jina alilokuja nalo. Yeye ni BWANA Yesu Kristo. Na mwanamke huchukua jina gani anapoolewa na mwanamume? Anachukua jina lake. Jina Lake ndilo analopewa bibi-arusi wakati anapomchukua Kwake.

Ufunuo 21:1-4.

*"Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita, wala hapana bahari tena.*

*Nami Yohana nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe.*

*Nikasikia sauti kubwa kutoka mbinguni ikisema, Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, Naye atafanya maskani Yake pamoja nao, nao watakuwa watu Wake. Naye Mungu Mwenyewe atakuwa pamoja nao, na atakuwa Mungu wao.*

*Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita."*

Ni ajabu iliyoje. Ahadi zote nzuri za Mungu zimetimizwa. Yote yatakuwa yamekwisha. Badiliko litakuwa limekamilika. Mwana-Kondoo na bibi-arusi Wake wamekaa milele katika ukamilifu wote wa Mungu. Ati utoe sifa ya jambo hilo? Ni nani awezaye kufanya jambo hilo? Hakuna mtu. Wazia jambo hilo? Uote juu yake? Soma kile Neno lisemacho juu yake? Ndiyo tunaweza kufanya hayo yote, hata hivyo tunaweza kujua tu sehemu yake iliyo ndogo sana mpaka itakapokuwa ni jambo halisi katika ule ufufuo wa kwanza.

*"Nami nitaandika juu yake Jina Langu Mwenyewe, lile JIPYA."*

Jina Langu Jipya. Wakati YOTE yatakapokuwa mapya, ndipo basi Yeye atajitwalia Mwenye Jina Jipya na Jina hilo litakuwa ndilo Jina la bibi-arusi pia. Jina hilo ni lipi, hakuna mtu anayethubutu kukisia. Ingebidi iwe ni ufunuo wa Roho uliotolewa kwa dhahiri sana hata hakuna mtu angethubutu kukana jambo hilo. Lakini hapana shaka atauacha ufunuo huo hadi siku ambayo Yeye anataka kulitangaza Jina hilo. Inatosha kujua ya kwamba itakuwa ni nzuri zaidi kuliko tunavyoweza kuwazia.

**Onyo La Mwisho Kwa Wakati Wote**

Ufunuo 3:13,

*"Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa."*

Kila wakati unaishia na onyo hili hili. Ni ombi la daima kwamba makanisa waisikie sauti ya Bwana. Katika wakati huu hilo ombi nii la nguvu zaidi kuliko katika nyakati zilizotangulia, kwa kuwa katika wakati huu kuja kwa Bwana kweli kunakaribia. Swali labda lingeweza kuzuka, "Kama kuna wakati mwingine baada ya huu, mbona dharura ya namna hii?" Jibu liko hapa. Wakati wa mwisho utakuwa ni mfupi—kazi ya haraka ya kumaliza. Na si kwamba jambo hili ndivyo lilivyo tu, lakini mtu hana budi kukumbuka daima ya kwamba katika macho ya Mungu wakati unapita haraka sana; naam, miaka elfu ni kama tu siku moja. Na kama Yeye anakuja katika masaa machache kama vile anavyouangalia wakati, Yeye hakika hana budi kutuonya kwa dharura yote na sauti Yake haina budi kusikia wakati wote katika mioyo yetu tuwe tayari kwa ajili ya kuja huko.

Loo, kuna sauti nyingi sana ulimwenguni—matatizo na mahitaji mengi sana yanayopaza sauti yapate kushughulikiwa; lakini kamwe hakutakuwako na sauti muhimu sana na yenye kustahili kushughulikiwaa kama sauti ya Roho. Kwa hiyo, "Yeye aliye na sikio la kusikia, na asikie yale Roho anayoyaambia makanisa."

MESSAGE hub online

www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7